epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Oktoba 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581832
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



# Kiharusi mtihani mgumu Muhimbili

• **Janabi:** Theluthi tunaowaona wamepooza, asilimia 60 waliolazwa Mloganzila ni wao, tumewaanzishia kitengo... *Ukurasa 2*

UKURASA WA 3

## **Wakili** aomba 'Afande' asomewe shtaka hospitalini

SAKATA la kesi inayomkabili Fatma Kigondo, maarufu Afande, jana...



UKURASA WA 4

## **Kamanda** Mssika atishiwa kurogwa kisa kufuatilia kesi

Katika sehemu ya pili jana, Kamanda mstaafu Abdallah...



UKURASA WA 19

## **Mahakama** Kenya yakataa kuingilia mchakato Bunge kumtoa Gachagua

KIONGOZI wa Chama cha...





Kikosi Maalumu cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kikiwa na Mwenge wa Uhuru katika lango la Marangu jana, tayari kwa kuupandisha katika Mlima Kilimanjaro kwa siku sita. **PICHA: MARY MOSHA**

## Biteko: Serikali imetoa ruzuku mitungi 400,000

UKURASA 3



# 15,000 waitwa usaili walimu nafasi 11,000

UK.2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA HATARI ZAIDI MAENEO HAYA UK.24 **KATUNI** UK.6

# Kiharusi mtihani mgumu Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

UGONJWA wa kiharusi unazidi kuwa tishio nchini. Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila imetangaza kuwa theluthi ya wagonjwa wa ubongo na mishipa ya fahamu inayowahudumia kila siku, ni wenye matatizo ya kupooza.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Prof. Mohamed Janabi ana lingine la ziada; asilimia 60 ya wanaolazwa kila siku katika wodi ya magonjwa yasiyoambukiza, ni wagonjwa wa kiharusi. Prof. Janabi alitoa ufafanuzi huo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, akisisitiza kuwapo ongezeko kubwa la wagonjwa wa kiharusi hospitalini huko.

Alisema kutokana na hali hiyo, hospitali imeanzisha Kitengo cha Kiharusi (Stroke Unit), akibainisha kuwa katika kipindi cha miaka miwili (2022-2024), Kitengo cha Ubongo na Mishipa ya Fahamu kimehudumia wagonjwa wa nje 10,271. Kati yao, nusu wanaugua kiharusi.

Vilevile, bingwa huyo wa maradhi ya moyo, alisema kuwa katika kipindi hicho tajwa, wagonjwa wa kifafa waliohudumiwa ni zaidi ya 334 na wanaoonwa ni walio katika umri mchanga hadi wa utu uzima.

Alisema hospitali hiyo iliona kuna umuhimu wa kuanzishwa kwa kitengo hicho; hivi sasa ni maalumu kwa ajili ya kiharusi kutokana na kasi yake. Alibainisha kuwa kati ya wagonjwa 10 wanaougua mfumo wa mishipa ya fahamu na ubongo, watano hadi sita wana kiharusi.

"Kitengo cha Ubongo na Mishipa ya Fahamu awali kilikuwa kinaona wagonjwa 50 katika kliniki, lakini baada ya kuhamia huku, wanaonwa wagonjwa 150. Utaona ukubwa wa tatizo kwa miaka miwili na waliolazwa ni wastani wa wagonjwa 2,953.

"Isivyo bahati, huu ugonjwa (kiharusi) unaingia katika magonjwa yasiyoambukiza (NCD) na duniani wagonjwa takribani milioni sita hufariki dunia kila mwaka," alifafanua Prof. Janabi.

Alisema serikali imeendelea kuboresha huduma za kitengo hicho, wakipatiwa fedha kutokana na mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19, nao wanatoa huduma za kibingwa na za kibobezi za kiuchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wanaofika kwa ajili ya kupata matibabu hayo. "Idadi kubwa ya wagonjwa wa kiharusi tunaowaona ni wanaougua presha na kisukari. Baada ya kuona tatizo ni kubwa, tumeanzisha 'Stroke Unit', ili kupunguza madhara ya ugonjwa huu ambayo yanahitaji huduma ya dharura.

"Magonjwa ya kiharusi huchangia asilimia kubwa kwa upande wa wagonjwa wa ndani na wagonjwa wa nje ambapo zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa wanaolazwa kila siku katika wodi ya magonjwa yasiyoambukiza, ni wagonjwa waliopata kiharusi. "Kiharusi kipo cha aina mbili: 'Ischemic stroke' (mishipa imebana) na 'hemorrhagic stroke' (mishipa imepasuka). Sasa ukiwa na wagonjwa 10 wenye aina hii ya pili, utawapoteza saba au wanane, watapoteza maisha. Ukipata aina ya kwanza, mgonjwa akifika kwa wakati utaweza kuwaokoa wanane hadi tisa.

"Lakini mtu anakuja na kiharusi, kisukari, uzito uliopitiliza na kiharusi, maana yake tafuta sababu. Kitengo hiki kina uwezo wa kuhudumia wagonjwa 10 kwa wakati mmoja. Tunaweza kutoa damu ya kuyeyusha damu iliyoganda kichwani, ila tuwe wazi bei, ni kubwa, Njia kubwa, chukua kinga ukiwa na kisukari, presha, tumia dawa na pili badili mtindo wa maisha," alisema.

Katika kitengo hicho, Prof. Janabi alisema utoaji huduma hutegemea wataalamu tofauti, wakiwamo wa moyo na kwamba kwa ambao wanaugua, ni hatari kufanyiwa huduma ya 'massage' na badala yake, alisisitiza itumike njia ya fiziotherapi.

"Wagonjwa wetu wa kiharusi hatuwafanyii 'massage' badala yake ni kuwafanyia mamacheza au fiziotherapi, kwa sababu 'massage' hufanya misuli yao kusinyaa zaidi, ukishafanya 'massage', mtu atajisikia mwili kulegea na kulala, hii haimfai mwenye kiharusi," alisema Prof. Janabi.

Alisema kitengo hicho pia kinatoa huduma kwa walio na kifafa kwa watu wazima. Kwa kipindi cha takribani miaka miwili hadi sasa, wamehudumia wagonjwa wa ndani 338 katika kipindi cha Oktoba 2022 hadi Septemba 2024 na wagonjwa wa nje walikuwa 4,850.

"Lengo kuu ni katika matibabu ya kisasa hata wanaougua kifafa wataweza kutibiwa kwa kufanyiwa upasuaji na si kutegemea tiba ya vidonge pekee. Ninashauri watu wabadili mtindo wa maisha, watembee kilomita zisizopungua sita kwa siku, yaani hatua 10,000 kila siku, si lazima uende 'gym'.

"Jamii ihimili msongo wa mawazo kwa sababu mishipa ya fahamu huathiriwa pakubwa, njia rahisi ya kukabiliana ni kufanya mazoezi, mshirikishe unayemwamini katika matatizo yako, fanya vipimo, angali mara mbili au mara moja kwa mwaka, au miaka miwili itategemeana," alishauri Prof. Janabi.

Alisema kitengo hicho pia kinahudumia wagonjwa wenye changamoto za kushindwa kutembea, magonjwa ambukizi ya mishipa ya fahamu na magonjwa yatokanayo na mifumo kinga (Autoimmune Disease).

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa kitengo hicho wamefanikiwa kupunguza madhara kwa wagonjwa wenye kiharusi kwa kuwa wagonjwa hao kwa sasa wanakaa hospitalini kwa muda mfupi, wanapata tiba ya magonjwa ambukizi kwa haraka na usimamizi maalumu wa mazoezi tiba. Bingwa wa Matibabu ya Ubongo na Mishipa ya Fahamu hospitalini huko, Dk. Mohamed Mnacho, alisema kiharusi kwa kiwango kikubwa kwa watoto sababu kuu ni wanaougua magonjwa ya kurithi kama vile selimundu na magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo.

Alisema kwa watu wazima sababu kuu ni mbili ambayo ni presha na kisukari na wengi wanaougua ni umri kuanzia miaka 40 na kwamba wanaotumia vilevi kupitiliza, wako hatarini kupata kifafa na kiharusi kwa sababu huzalisha sumu kuathiri mfumo wa fahamu. "Kemikali za pombe huathiri mfumo wa ubongo, ndio maana mtu hukosa uwiano wa ubongo, ikiendelea seli zitakufa, ataanza kutetemeka, kuchanganyikiwa, kusahau na kuwa chanzo cha kifafa. Kama ni lazima sana kunywa pombe, kunywa chupa moja," alionya bingwa huyo.

# Usaili maelfu nafasi 11,000 za walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAELFU ya waombaji nafasi za kazi za ualimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wameitwa kwenye usaili kwa ajili ya ajira 11,000 ambao unatarajiwa kuanza Oktoba 23, mwaka huu.

Julai mwaka huu, serikali ilitangaza nafasi hizo za kazi za walimu wa shule za msingi na sekondari.

Awali, waombaji wa kada hiyo walikuwa wakiomba kupitia mfumo wa ajira wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na hakukuwa na usaili wa aina hiyo. Waombaji walikuwa wakiomba kwenye mfumo huo na baada ya uchambuzi, wenye sifa walikuwa wakipangiwa vituo vya kazi.

Hata hivyo, nafasi hizo za ajira safari hii jukumu limefanywa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Katika tangazo lililotolewa na sekretarieti hiyo la kuwaita kwenye usaili waombaji linabainisha kuwa usaili huo utaendeshwa kuanzia Oktoba 23 hadi Novemba 16, mwaka huu na hatimaye kuwapangia vituo vya kazi kwa watakaofaulu.

Ratiba ya usaili wa mchujo itakuwa Oktoba 23, mwaka huu, saa 1:00 asubuhi kwa walioomba ualimu daraja la IIIA na elimu ya awali na utafanyika kwenye vituo mbalimbali kulingana na anwani ya mwombaji ya sasa.

Novemba 11 hadi 16, mwaka huu utafanyika usaili wa mahojiano kwa waombaji wa nafasi hizo kwenye mikoa ambayo wasailiwa walichagua na kuthibitisha kuwa wameomba kazi katika mkoa huo na kwamba vituo husika watajulishwa kupitia akaunti zao za Ajira Portal na tovuti ya sekretarieti hiyo.

Pia kwa upande wa nafasi ya Mwalimu Daraja la IIIB somo la Bailojia, Kemia, Jiografia na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), usaili wa mchujo utafanyika Oktoba 25, mwaka huu, saa 1:00 asubuhi kwenye vituo mbalimbali kulingana na anwani za sasa za waombaji husika.

Katika usaili wa mahojiano kwa nafasi hizo, kwa Novemba 13, mwaka huu, saa 1:00 asubuhi utafanywa kwa nafasi ya Mwalimu daraja IIIB wa somo la Bailojia na Kemia huku Novemba 15 itakuwa mwalimu wa daraja hilo wa Jiografia na Novemba 18 Mwalimu wa TEHAMA.

Kadhalika, usaili wa mchujo kwa Mwalimu daraja IIIB wa Historia, Shule za Msingi, Kiswahili, Elimu ya Awali, Uraia watafanyiwa usaili Oktoba 27, mwaka huu, na usaili wao wa mahojiano utafanyika kwa mwalimu wa Historia Novemba 15, mwaka huu, Kiswahili, Uraia na Elimu ya Awali (Novemba 16) na Mwalimu wa Shule ya Msingi (Novemba 19). Oktoba 31, mwaka huu, utafanyika usaili wa mchujo wa nafasi ya Mwalimu wa Daraja IIIC wa Jiografia na usaili wa mahojiano utafanyika Novemba 15.

Novemba 2, utafanyika usaili wa mchujo nafasi ya Mwalimu wa Daraja la IIIC wa Historia na usaili wake wa mahojiano utakuwa Novemba 15. Nafasi ya Mwalimu wa Fasihi ya Kiingereza daraja la IIIC usaili wa mchujo na mahojiano utakuwa Novemba 16, mwaka huu.

Hata hivyo, usaili wa mchujo kwa Mwalimu daraja la IIIC wa Somo la Baiolojia, Tehama, Uchumi utafanyika Novemba 6, mwaka huu, wakati wa mahojiano utakuwa Novemba 14 kwa Mwalimu wa Baiolojia, Novemba 15 Mwalimu wa Uchumi na Novemba 18 Mwalimu wa TEHAMA.

Usaili wa Mchujo kwa Mwalimu daraja la IIIC wa Somo la Kemia, Shule za Msingi, Elimu Maalum, Uraia na Kilimo utakuwa Novemba 8, mwaka huu, huku usaili wa mahojiano utakuwa Novemba 13 utakuwa kwa Mwalimu wa Kemia, Uraia (Novemba 16), Kilimo (Novemba 18), Shule za Msingi na Elimu Maalum (Novemba 19).

Aidha, waombaji wa Mwalimu daraja la IIIB wa Fizikia wao watafanya usaili wa mahojiano Novemba 14, mwaka huu huku Mwalimu wa daraja IIIB wa Hisabati utafanyika Novemba 12, mwaka huu sambamba na Mwalimu daraja IIIC wa Fizikia na Hisabati.

Kwa Mwalimu wa Fasihi ya Kiingereza daraja la III B, usaili utafanyika usaili wa mahojiano Novemba 16, mwaka huu na Novemba 18 utafanyika kwa waombaji wa Mwalimu daraja la IIIB wa Kifaransa, Somo la Biashara, Lishe, Ushonaji na Kilimo sambamba na Mwalimu daraja la IIIC wa somo la Biashara na Maabara.

Novemba 19, utafanyika wa usaili wa mahojiano kwa nafasi ya Mwalimu elimu maalum IIIA, Mwalimu daraja IIIB Somo la Biashara, Elimu maalum na Mwalimu wa daraja IIIC somo la Biashara.

Hivi karibuni, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu alisema kuwa azma ya serikali ya kupeleka kibali cha ajira kwa kada za afya na elimu katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni kuhakikisha serikali inapata watumishi wenye sifa, ili kuongeza tija na ubora katika utumishi wa umma.

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa usaili huo utaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA ARDHI NA 22 YA 2022**

**BITALIHO RUHERE ..............................................................MDAI**

**DHIDI YA**

1. LAZARO CHIBAGO LECHIPYA
2. DAVID C. MAZIKU
3. THE REGISTERED TRUSTEES OF AFRICA BENEDICTINE SISTERS OF ST. AGNES CHIPOLA
4. THE REGISTERED TRUSTEES OF CHRIST TO ALL PEOPLE CHURCH
5. YUSUPHU H. ABUU
6. DICKSON EVALIST
7. NICKSON JACKSON MDOL
8. DEODAS PIUS
9. EMMANUEL JACKSON ..................**WADAIWA**
10. MOSES REBEN
11. FREDY OSWADY
12. MATHAYO BWELI
13. ARON EXAUDY
14. EMMANUEL
15. PATRICE WAMILY KUGULULYE
16. JAMES RAPHAELY KALALU
17. IMAN ONESMO MAHELELA
18. MAGOMBA
19. PLOTUS
20. NEEMA JEREMIA
21. OMARY

**KWA:**

1. LAZARO CHIBAGO LECHIPYA
2. DAVID C. MAZIKU
3. THE REGISTERED TRUSTEES OF AFRICA BENEDICTINE SISTERS OF ST.AGNES CHIPOLA
4. THE REGISTERED TRUSTEES OF CHRIST TO ALL PEOPLE CHURCH
5. YUSUPHU H. ABUU
6. DICKSON EVALIS
7. NICKSON JACKSON MDOL
8. DEODAS PIUS
9. EMMANUEL JACKSON
10. MOSES RUBEN
11. FREDY OSWADY
12. MATHAYO BWELI
13. ARON EXAUD
14. EMMANUEL
15. PATRICE WAMILY KUGULULYE
16. JAMES RAPHAEL KALALU
17. IMAN ONESMO MAHELELA
18. MAGOMBA
19. PLOTUS
20. NEEMA JEREMIA
21. OMARY

**POPOTE PALE WALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 22 YA 2022**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatolewa hukumu Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. E. E. KAKOLAKI, JAJI wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa nane (8:00) kamili Mchana Siku ya Ijumaa tarehe 8/11/2024.

HIVYO; Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyinyi au wakili wenu kuwepo.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 9/10/2024

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakiponda kokoto katika eneo la Mbuyuni, Manispaa ya Kinondoni juzi, kwa ajili ya kuziuza ili kujipatia riziki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Biteko: Serikali imetoa ruzuku mitungi 400,000

**Na Grace Mwakalinga**

SERIKALI imetoa ruzuku kwa mitungi zaidi ya 400,000 ya gesi ya kupikia (LPG), ambayo itaanza kugawiwa kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini mwishoni mwa mwaka huu.

Lengo la kufanya hivyo ni kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ambayo kwa sasa inapigiwa chapuo, ili kulinda afya za wananchi na kutunza mazingira.

Ikumbukwe kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia yanaokoa muda, unatumika muda wa saa mbili kwa wiki kupika, huku nishati chafu kama vile kuni na mkaa ikitumia saa saba kwa wiki.

Katika Kongamano la Tisa la Nishati na Biashara Afrika, lililofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, lijadili namna nchi hizo zitakuwa na nishati ya uhakika ya umeme.

Akifungua kongamano hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema ugawaji wa Mitungi ya gesi yenye ruzuku ni hatua ya serikali katika kuhamasisha matumizi ya nishati ya kupikia.

Kuhusu sababu ya kwa kuelekeza nguvu ya kutumia nishati ya gesi LPG kuliko nyingine, alisema mkakati wa serikali kuhamasisha matumizi ya nishati ya kupikia unahusisha vyanzo vyote vikiwamo vya umeme jua na mkaa mbadala na wanaendelea kuweka mazingira rafiki ili kutumika.

"Serikali inahamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwamo inayotokana na umeme jua, mkaa mbadala na gesi ambavyo tumetoa ruzuku na wananchi watapata mitungi kwa bei nafuu, kuhusu usalama wa gesi nakiri haina madhara na hadi sasa hakuna visa vyovyote vilivyoripotiwa tungu tuanze kuhamasisha matumizi yake," alisema Dk. Biteko.

Tanzania imekuwa nchi kinara katika uhamasishaji wa matumizi ya nishati mbadala, pia imefanikiwa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kwenye maeneo mbalimbali.

Dk. Biteko alisema hadi kufikia mwezi Desemba, mwaka huu, vijiji 12,000 vitaunganishwa na huduma ya umeme kupitia Wakala wa Huduma za Nishati Vijijini (REA).

Aidha, Tanzania ina mchango wa kuhakikisha watu milioni 300 katika Bara la Afrika wataunganishwa na huduma ya umeme ifikapo mwaka 2030.

Alisema mapema mwezi Januari 2025, Tanzania itaandaa mkutano wa kujadili masuala ya nishati safi na upatikanaji wa umeme kwenye nchi za Afrika na miongoni mwa majadiliano ni pamoja na kupata namna ya kufanikisha kuwaunganishia nishati ya umeme watu milioni 300 kwenye nchi zote.

"Tumepata heshima kuandaa mkutano mkuu wa nchi za Afrika kujadili masuala ya nishati safi ya kupikia na umeme, ni baada ya kuona tumefanya vizuri katika kutekeleza miradi mbalimbali ambayo mingine imekamilika na tubakia na akiba ya umeme ambao tunaweza kuuza kwenye mataifa mengine," alisema Biteko.

Msimamizi wa Mkutano huo, Dk. Patricia Laverley ambaye ni Meneja Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), alisema wanaungana na serikali kutekeleza miradi mbalimbali inayohusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Aidha, alisema wanafanya hivyo ili kumwezesha mwanamke kutumia nishati safi kulinda afya yake na kuokoa muda ambao mara nyingi anautumia kutafuta nishati isiyo rafiki wa mazingira. Mwenyekiti wa Nishati, Mabadiliko ya Tabianchi na Uchumi wa Kijani kutoka Benki Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dk. Kevin Kariuki, alisema watashirikiana na wadau wengine kupiga debe jitihada zinazofanywa na serikali kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Rais Samia Suluhu Hassan ameibeba ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika, huku Tanzania ikiweka malengo ya kufikia asilimia 80 ya Watanzania ifikapo 2030.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

# Wakili Madeleka ataka 'Afande' kusomewa mashtaka hospitalini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SAKATA la kesi inayomkabili Fatma Kigondo, maarufu Afande, jana lilichukua sura mpya baada ya wakili wa upande wa mlalamikaji, Peter Madeleka, kuomba Mahakama ya Wilaya ya Dodoma kumsomea mashtaka katika hospitali aliyolazwa ili hatua zingine za kisheria ziendelee.

Kigondo anakabiliwa na shtaka la kubaka kwa kundi kinyume cha kifungu cha sheria namba 131 A kifungu kidogo cha pili ambacho kinasema anayewasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji na yeye anahusika kwenye ubakaji wa kundi.

Mshtakiwa huyo ambaye alipaswa kufika mahakamani Oktoba 7, mwaka huu, kusikiliza shtaka linalomkabili, hakufanya hivyo kwa madai yaliyotolewa na wakili wake Sedrick Mbunda kuwa ni mgonjwa.

Baada ya kauli hiyo Wakili Madeleka, alitoa maombi hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, Nyambuli Tungaraja.

Katika maombi yake, Wakili Madeleka, aliiomba mahakama hiyo kutia saini malalamiko yaliyowasilishwa na mlalamikaji Paul Kisabo, mahakamani hapo dhidi ya Kigondo ili yatumike kama hati ya mashtaka.

"Mweshimiwa Hakimu tunaiomba mahakama yako tukufu kusaini malalamiko haya tuliyowasilisha dhidi ya Fatma Kigondo ili yatumike kama hati ya mashtaka na baada ya kusainiwa mshtakiwe asomewe mashtaka yake katika hospitali yoyote alipo bila kujali anaumwa ugonjwa gani. Iwe Muhimbili, Benjamini Mkapa, Bugando au sehemu yoyote ili hatua zingine za kisheria ziendele," alidai Madeleka.

Baada ya maombi ya wakili huyo, Hakimu Tungaraja aliahirisha kesi hiyo hadi kesho atakapotoa uamuzi baada ya kupitia baadhi ya mifungu vya sheria.

Aidha, akizungumza nje ya mahakama, Wakili Madeleka alisema jana walipanga kupeleka maombi yao ya marejeo Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma ili ikaangalie mwenendo wa shauri hilo hadi sasa kwa sababu kumekuwa na hila na fitina nyingi.

"Mara hakimu aliyekuwapo kahamishwa mara wanasema hakimu hajapangiwa, mara hakimu aliyepangiwa anasema mahakama si kazi yake kwenda kumkamata mshtakiwa kwamba dhamana ni haki ya mshtakiwa, yaani vitu ambavyo havielewki. "Mahakama inakuwa inajichanganya sasa tunaona badala ya kupoteza muda na rasilimali fedha tunakuwa tunakuja hapa kwa vitu visivyoeleweka ni bora twende kwa watu wanaojielewa wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma," alisema.

Alisema Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma itafanya mapitio kwenye kesi hiyo ili kuona mwenendo wa kesi hiyo kama unakwenda kwa mujibu wa sheria ama vinginevyo na ikioneka mahakama inakiuka sheria Mahakama Kuu inayo mamlaka ya kutoa maelekezo nini kifanyike ili haki iweze kutendeka kwa pande zote mbili," alisisitiza.


## CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)

## TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA (Marudio)

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) anawatangazia nafasi ya ajira kama ifuatavyo:-

**1.0. AFISA MANUNUZI MWANDAMIZI (Nafasi 1)**

**1.1. Sifa na uzoefu**

- Kuajiriwa mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya Manunuzi au Ugavi kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na cheti kutoka katika Bodi ya Manunuzi au ugavi
- Awe na uzoefu wa kufanya kazi za manunuzi au ugavi kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5)
- Awe na ufahamu wa matumizi ya kompyuta

**1.2. Kazi za kufanya.**

- Kusimamia utekelezaji wa mpango wa ununuzi
- Kuratibu uandaaji wa mikataba ya ununuzi wa vifaa
- Kushauri kuhusu utekelezaji wa mikabata na ukaguzi
- Kusimamia uzingatiaji wa Kanuni za Manunuzi
- Kusimamia ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za soko kwa baadhi ya bidhaa
- Kuratibu tafiti mbalimbali zinazohusu manunuzi
- Kuandaa na kutoa mikataba iliyoidhinishwa nna kusimamia utekelezaji wake
- Kuandaa na kupendekeza njia nzuri ya ufanisi wa Ununuzi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya Chama
- Kuratibu utoaji wa elimu ya manunuzi kwa watumishi wa Chama
- Kusimamia uondoaji wa vifaa kwa njia ya zabuni
- Kuratibu shughuli za ufunguzi wa zabuni
- Kufanya kazi nyingine za fani yake atazopangiwa na mkuu wake wa kazi

**1.3. MASHARTI YA JUMLA**

- Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 45
- Waombaji wa nafasi hii wahakikishe wanaambatanisha nakala ya Vyeti vya Taaluma na Ujuzi kutoka kwenye Vyuo na Taasisi zinazotambuliwa na Serikali
- Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa na Mwanasheria/wakili
- Waambaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba za Simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini ya kuaminika
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 31 Oktoba 2024

MUHIMU: Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya taaluma na ujuzi na picha ya pasport.

**1.4. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji wenye sifa zilizotajwa watume maombi yao kwa:
**KATIBU MKUU**
**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)**
**S.L.P 16097**
**DAR ES SALAAM**

..............................
**Rashid M. Mtima**
**KATIBU MKUU – TALGWU TAIFA**

KAMANDA MSSIKA

# Atishiwa kurogwa kisa kufuatilia kesi

Na Romana Mallya

**Katika sehemu ya pili jana, Kamanda mstaafu Abdallah Mssika alitaja matukio mambo manne ambayo hatoyasahau katika utumishi wake wa miaka 40 ndani ya Jeshi la Polisi, ikiwa ni pamoja na kuripotiwa isivyo sahihi na vyombo vya habari kwamba alitaka kununua cheo cha Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP). Endelea na sehemu ya mwisho ya mazungumzo yake na Nipashe, akisimulia namna alivyokabiliana na vitisho, ikiwamo kurogwa, katika kutekeleza majukumu yake.**



Kamanda Mstaafu Abdallah Mssika

KAMANDA Mssika anasema, "Hakuna meli inayokosa nanga. Matishio ni mengi na hasa wakati nikiwa katika nafasi ya RCO.

"Nilipata vitisho vingi nikiwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mara, Mwanza na Dodoma kabla sijapangiwa majukumu ya RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) Rukwa, Lindi, Shinyanga, Kagera na mwanzilishi Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

"Kujibu swali lako, vitisho vya moja kwa moja nikiwa nafasi za RCO mikoa hiyo vilikuja kwa muundo huu, 'Hili umelionea, nitahakikisha huwi RCO tena hapa. Nitahakikisha matukio yote ambayo umeyafanya na mahali ulikofanya rushwa tutaweka hadharani. Kesi fulani usiifuatefuate'.

"Matishio mengine ya ana kwa ana yalikuwa yakifanywa na mahabusu walioko tayari gerezani na wanaoandaliwa kupelekwa gerezani.

"Yalikuja kwa mtazamo huu, 'Unajifanya wewe ndiye unajua kufuata taratibu, nitahakikisha nikitoka ama wewe mwenyewe ama anayekuhusu au mali zako nimeshatoa maagizo watu wafuatilie," anasema.

### WIZI SHULENI

Kamanda Mssika anakumbuka kesi ya wizi ya mamilioni ya shilingi katika Shule ya Sekondari Weruweru, mkoani Kilimanjaro, ambako mhasibu shuleni huko alituhumiwa kughushi saini ya aliyekuwa Mkuu wa Shule hiyo na kuitumia katika vocha za shule.

"Upelelezi ulianza akiwa ameshatoroka, ilituchukua muda mrefu. Chanzo cha taarifa kutoka Bagamoyo kilitutaarifu alikuwa amekimbilia huko, tukaandaa safari kupitia Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na polisi wa eneo husika, tukaenda kwa siri.

"Tukiwa Bagamoyo, mbinu ya upelelezi tuliyotumia, kwa sababu nilikuwa mzoefu katika masuala ya uuguzi, tulitumia mavazi ya uuguzi na vifaa vya hospitalini kuanza upelelezi wa tukio hili.

"Taarifa ikaja yuko kijiji kimoja kwa nyanya wake (bibi). Wakati huo utakumbuka taarifa tulikuwa tunazikusanya tukiwa na kofia kama wauguzi na madaktari.

"Utekelezaji eneo la tukio tulikwenda kiaskari, tukavamia nyumba ya bibi yake. Bibi huyo aliaminika kipindi hicho kuwa kati ya viongozi wanaojihusisha na uchawi katika eneo lile.

"Tulipofika eneo la tukio nyumbani kwa bibi huyo, tulipoingia katika sebule yake, tulikuta ndege wamekaushwa na miguu ikining'inia. Alishtuka kutuona. Swali la kwanza ni wapi aliko Omar Madongo? (mtuhumiwa).

Kutokana na mshtuko, bibi huyo hakuwa na majibu, lakini kijana aliyetuongoza kwenda hapo akanieleza kuwa mtuhumiwa hakuwa katika nyumba hiyo, bali alikuwa amejificha katika nyumba nyingine na walipoivamia hakukuwa na dalili za mtu kuishi humo.

"Ng'ambo ya barabara kulikuwa na gari ambalo mtuhumiwa alitoroka nalo Moshi. Kulikuwa na vibanda vitatu, kimoja kimezibwa sehemu zote na sehemu ya juu iko wazi, liliwekwa lile gari.

"Alinunua nyumba akaitengeneza vizuri ili gari lienee humo, hata mpitanjia asiweze kuona. Tulibomoa nyumba, gari likiwa ndani na lilikuwa na mafuta yaliyojaa na lita zingine 20 kwenye dumu. Mtuhumiwa alikuwa maarufu mjini Moshi na Arusha kwa sababu alikuwa na fedha.

"Tukiwa mjini Bagamoyo, tulipokea simu kutoka kwa ndugu yake akituarifu, 'mtuhumiwa yupo Kituo cha Polisi Magomeni, Dar es Salaam' na tulipokwenda tulimkuta na ndipo tulipomchukua kwenda naye Moshi (ilikokuwa kesi yake)," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema kuwa kutokana na umaarufu wa mtuhumiwa huyo, alipokea vitisho kutoka kwa watu (bila kuwataja), walimtishia na hata kujaribu kumkatisha tamaa kwamba atahamishwa eneo la kazi.

"Vilikuja kwa njia mbalimbali. Mpaka vitisho vya uganga. Wakati tunakwenda mahakamani, watu walikuwa wanatupa vitu kwenye njia niliyokuwa ninapita kwa lengo la kunitishia na kunikatisha tamaa, lakini hatimaye alihukumiwa kifungo chini ya Jaji Kileo," anasimulia.

### JESHI KULALAMIKIWA

Kamanda Mssika anasema anaweza asiwe na majibu ya moja kwa moja kwanini watu hulalamikia Jeshi la Polisi kutokana na utendaji wa askari wake.

"Jeshi la Polisi lipo kwa ajili ya kulinda raia na mali zao. Kunapotokea malalamiko ya aina yoyote, kwanza ni pongezi kwa wananchi kwa jumla, lakini ni pongezi kwa wanaolalamika.

"Majibu ya moja kwa moja kwamba ni sababu ipi inayopelekea, ushauri wangu kila malalamiko yajadiliwe kulingana na tukio husika.

"Malalamiko yanapojitokeza, hasa upande mmoja ni lazima yawe na majibu ya pande zote mbili, wananchi wanalalamika, hii ni kwa ujumla. Kama wanalalamika mfano kesi haziendi sawa au kukamatwa isivyo, mimi binafsi ninaona malalamiko ya jumla yakizingatiwa kuna uwezekano kupata matokeo ya sababu ya kijumla.

"Nikizungumzia uzoefu, malalamiko mengi yanayotolewa yanafikishwa polisi, wanayapokea na kufanya uchunguzi mpaka kufika hatua ya mwisho. "Tumelalamika namna hii, polisi imelishughulikia na kuchunguza na kubaini moja, mbili, tatu. Hiyo ikifanyika, inaweza kuondoa mawingu mbalimbali kwamba mrejesho unafanyika," anasema.

Kamanda Mssika anasema kwa uzoefu wake katika kazi hiyo, malalamiko yanayowasilishwa kwa Jeshi la Polisi ni yale ambayo tukio limetokea leo, mtu amebaki nalo hakulitolea ripoti kwa wakati mwafaka.

Anasisitiza kwamba polisi kuna kitengo maalumu cha uchunguzi wa malalamiko ya polisi yanayofikishwa huko.

Kamanda Mssika anasema maboresho yanayofanywa Jeshi la Polisi katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ni makubwa.

"Tumeshuhudia kuundwa Tume ya Haki Jinai, ninaamini imempelekea Rais ya ziada ambayo yameanza kufanyiwa kazi.

"Jeshi la Polisi katika usasa ndiko lilikojikita. Linashirikiana kimataifa, hivyo huwezi kubaki nyuma wakati majeshi mengine ya kimataifa yanakwenda mbele kwa teknolojia," anasema.

Kamanda Mssika anasisitiza hatua hiyo iendelee na kushauri Programu ya Polisi Jamii nayo iboreshwe zaidi.

### WALIOKALIA KITI

Kamanda Mssika anasema, "Kwa watendaji Jeshi la Polisi, jamii uliyonayo ukiwa kwenye kiti ndiyo hiyohiyo itakupokea ukiondoka katika kiti.

"Hivyo, polisi jamii inabidi ianze nyumbani, ndani ya Jeshi la Polisi, uhusiano, utekelezaji wa kweli na ushirikiano na wananchi uwe endelevu.

"Uelewa wa wananchi ni mkubwa, wanapima kwenye mizani utendaji wa polisi na malalamiko hayaji Jeshi la Polisi kwa jumla, yanalenga kwa baadhi ya matukio ambayo hayaripotiwi na kurekebishwa," anasema.

Kamanda Mssika anashauri wasiitwe kufafanua malalamiko yao kama tuhuma, bali zitumike kama fursa kuzifanyia kazi na kuzitafsiri kwanini zimejitokeza na kuziondoa.

"Unapofikiri haliwezi kuhesabika, linahesabika hatua kwa hatua na huwezi kujua kama linahesabika mpaka hapo umeondoka ndani ya jeshi, upo uraiani," anasema.

Kamanda Mssika pia anashauri watendaji ndani ya jeshi hilo kuzingatia utendaji wa haki wanapokuwa katika meza zao na si kuchanganya na tamaa ya aina yoyote, yao binafsi au kufanya kwa niaba.

"Mbegu unayoipanda leo, inakuja kujibu ukishaondoka. Uhusiano unaojenga leo uwe wa kutenda haki kwa maana kama mhalifu, haki yake apatiwe kwa yale aliyofanya.

"Ukitenda haki kila mtu anajua 'hii ilikuwa haki yangu, kama ni kufungwa mimi ni mhalifu'. Ukitenda haki ni njia moja wapo ya kuimarisha uhusiano kupitia programu ya polisi jamii," anasema.

Kamanda Mssika hadi kustaafu kwake, ana nishani ya vita ya mstari wa mbele, nishani ya utumishi mrefu na tabia njema na nishani ya utumishi uliotukuka ndani ya Jeshi la Polisi.

Hivi sasa anaandaa kitabu ambacho pamoja na mambo mengine, kinahusu maisha yake kwa ujumla katika ajira, kuanzia kazi aliyofanya hospitalini Muhimbili, Jeshi la Polisi na anachofanya kwa sasa.

## HABARI KITAIFA




# Mwinyi apongeza CRDB kuongoza mikopo ya nyumba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi amepongeza Benki ya CRDB kwa mchango wake mkubwa katika utoaji mikopo ya nyumba, akitoa wito kuongezwa juhudi zaidi ili kuwawezesha watu wengi kupata makazi bora.

Alitoa pongezi hizo jana alipofungua mkutano wa 40 wa mwaka wa Umoja wa Afrika wa Fedha za Makazi (AUHF) na Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) unaofanyika visiwani hapa kuanzia tarehe 14 hadi 18 Oktoba mwaka huu, Benki ya CRDB ikijiunga tena na shirika hilo la barani.

"Kuanzia Juni 2024, nimeambiwa kuwa, idadi ya benki za biashara na taasisi za kifedha zinazotoa mikopo ya nyumba ilikuwa 31, zikiwezesha jumla ya Sh. bilioni 625, sawa na dola za Marekani milioni 234.3 kama mkopo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba.

"Ingawa hii inaonesha tumepiga hatua kubwa, juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha kila mtu anapata fursa ya mikopo ya nyumba kwani hii ni njia sahihi ya kumiliki nyumba nzuri na kuishi kwa heshima," alisema Rais Mwinyi.

Alisisitiza kuwa Benki ya CRDB ikiongoza katika utoaji mikopo ya nyumba kwa asilimia 34.4, ni mfano mzuri kwa washindani wake ambao wanahitaji kuja na mikakati iliyobuniwa ili kufikia wateja wengi zaidi na hivyo kuchangia zaidi katika sekta ya mikopo ya nyumba na uchumi kwa ujumla.

Rais Mwinyi alizitaka benki za biashara na taasisi za kifedha kutoa ushauri wao bora kuhusu namna ya kuongeza idadi ya watu wanaopata mikopo ya nyumba nchini.

Licha ya kuwa na idadi kubwa ya wakopeshaji nchini, Rais Mwinyi alisema Watanzania wengi hawawezi kufikia mikopo ya nyumba, hali inayowafanya kutumia muda mrefu kukamilisha ujenzi wa nyumba zao, jambo ambalo linafanya ujenzi kuwa ghali zaidi.

"Ninyi ni wataalamu katika eneo hili. Milango ya serikali iko wazi kukaribisha maoni yenu juu ya jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo. Tafadhali shirikianeni nasi ili kuzitatua na kuruhusu Watanzania wengi kadri iwezekanavyo waweze kupata mikopo ya nyumba," aliagiza Rais Mwinyi.

Kuhusu mchango wa Benki ya CRDB, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Awali wa benki hiyo, Bonaventura Paul, alisema kuwa, "hadi Juni mwaka huu, tulikuwa tumetoa jumla ya Sh. bilioni 208.34, zikinufaisha wateja 1,628 na uwezo wetu ni zaidi ya hapo, hivyo tunakaribisha wateja wengi zaidi kuchangamkia fursa ya kujenga na kumiliki nyumba nzuri.

"Katika Benki ya CRDB tunatoa mikopo ya nyumba kwa ajili ya makazi ya biashara. Tuna uwezo wa kutosheleza mahitaji na matarajio ya wateja wetu. Tunakaribisha yeyote anayeweza na anayeshawishika kwa mikopo," Bonaventura alikaribisha wateja.

Alisisitiza umuhimu wa kuvutia rasilimali zaidi kwa kuwa taasisi za kifedha zilizopo zinaweza kutoa mikopo ya nyumba 200,000 tu kwa mwaka, na kuacha nchi ikiwa na upungufu wa nyumba milioni tatu ambao umekuwapo kwa muda mrefu bila kushughulikiwa.

Alisema ikiwa hakuna hatua bunifu zinazochukuliwa, nchi itakumbana na upungufu huo kwa miaka mingi zaidi na kuathiri hata vizazi vijavyo.

Takwimu rasmi za mikopo ya nyumba zinaonesha kuwa wastani wa mkopo wa nyumba kwa kila mkopaji kufikia Juni 2024, ulikuwa Sh. milioni 104.8, sawa na dola 39,286.2, huku mahitaji ya makazi na mikopo ya makazi yakiwa juu nchini, changamoto zinazohitaji juhudi za pamoja kushughulikia.

"Ukosefu wa hati miliki kwa Watanzania wengi ni moja ya changamoto kubwa inayowafanya wengi kushindwa kupata mikopo ya nyumba. Serikali inapaswa kutafakari na kuona jinsi inavyoweza kushughulikia hali hii. Mara baada ya hili kushughulikiwa, wengi wataweza kukidhi vigezo vya mikopo inayotolewa," alisisitiza Bonaventura.

Utafiti unaonesha kuwa ni asilimia tatu tu ya Watanzania wana hati miliki, hivyo kukosa moja ya vigezo vya mikopo ya nyumba, na kuacha idadi kubwa ya watu wasio na sifa ambao wanalazimika kujenga nyumba kwa kutumia vyanzo vingine vya fedha, ujenzi ambao ni ghali zaidi.

Benki ya CRDB mwaka huu imejiunga tena na AUHF, umoja unaokusanya pamoja benki zinazotoa mikopo, taasisi za ujenzi, mashirika ya nyumba na mashirika mengine ya fedha za makazi kutoka nchi 17 barani Afrika ili kukusanya fedha za makazi ya bei nafuu na nyumba barani Afrika.

Mkutano wa mwaka huu, ambao AUHF imeshirikiana na Shirika la Kimataifa la Masoko Makubwa ya Mikopo (ISMMA), unalenga kuimarisha maendeleo ya soko, kuboresha ufanisi na kushughulikia changamoto katika masoko ya makazi barani Afrika ambapo upungufu wa makazi ni changamoto kubwa kwa nchi nyingi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA HUDUMA YA WAKALA WA AJIRA ZA WAFANYAKAZI (MADEREVA) NCHINI TANZANIA. NAMBA YA REJEA: 000000635**

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya uwakala wa ajira za madereva wenye uzoefu kwa ajili ya kampuni.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Ikiwa kama dhamira ya kampuni kuendeleza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa Raia wa Tanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, kampuni inalenga kuajiri raia wa Tanzania wenye uzoefu na weledi wa kuendesha magari ya aina mbalimbali (magari madogo na makubwa (mabasi madogo n.k.) yanayotumiwa na Mradi huo katika shughuli zake za kila siku katika eneo lote la Mradi kupitia fursa mbalimbali zinazopatikana katika mradi.

Kwa hivyo EACOP inatafuta huduma kutoka kwa (ma)kampuni inayoheshimika yenye rekodi ya uzoefu wa kuajiri na kutoa huduma za wafanyakazi inayolingana na mradi ya mafuta na gesi ili kutoa huduma za ajira za madereva waliohitimu vyema, wenye uzoefu na afya njema kwa ajili ya kuendesha magari ya KAMPUNI kwa kufuata sheria za KAMPUNI, taratibu, miongozo na mafunzo kuhusu usafiri wa nchi kavu pamoja na sheria na kanuni za Tanzania.

**Idadi ya wafanyakazi**

| Idara | Idadi | Mahali |
|---|---|---|
| Msimamizi wa Madereva | 1 | Ofisi za Dar Es Salaam |
| Msimamizi Msaidizi wa Madereva | 1 | Ofisi za Dar Es Salaam |
| Madereva | Takribani 94 | Dar es salaam au katika eneo la kazi kulingana na shughuli na mahitaji ya KAMPUNI |

**Jukumu na shughuli za msimamizi wa Dereva ni**

- Kusimamia madreva /mpango kazi wa kila siku wamadereva kwa kuzingatia matakwa ya EACOP.
- Kuhakikisha kuwa usafiri wowote unazingatia kwa usahihi JMP.
- Kuhakikisha magari yapo katika hali nzuri (ukaguzi wa kila siku, matengenezo ya mara kwa mara)
- Kuhakikisha madreva wanajali muda wa kupumzika na likizo ya madereva.
- Kufuata sera ya (dizeli/petrol)/ Nishati ya KAMPUNI.
- Kuhakikisha huduma zinatolewa kwa kukidhi viwango vya EACOP.
- Kuandaa mikutano na madereva (sanduku la vifaa, mkutano wa robo mwaka)
- Kusasisha/kuhuisha kanzidata kuhusu madereva na magari.
- Kushiriki katika mikutano yote inayohusishwa na shughuli za madereva.
- Kushiriki katika mkutano wa kila mwezi na kutoa ripoti za kila mwezi za magari madogo.

**VIGEZO MUHIMU VYA HUDUMA:**

**Makampuni au mashirika yanayoonesha nia yanakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Cheti cha usajili chaBRELA cha hivi karibuni (ambatanisha nakala)
- Cheti cha Uthibitisho wa mamlaka husika ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) nk.
- Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa Leseni Halali ya Biashara.
- Uthibitisho wa uzoefu katika kutoa huduma sawa na hii katika miradi au makampuni husiani ikiwa ni pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa hivi karibuni.
- Wasifu wa wafanyakazi wakuu watakaoshiriki katika mradi ikiwa ni pamoja na viwango vya Elimu, uzoefu, na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Unashauriwa kuwasilisha Ushahidi wa usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa Sera za Kupambana na Rushwa, Kupambana na Rushwa, Uzingatiaji na Haki za Kibinadamu.

Makampuni ambayo yana nafasi, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma Maombi pamoja na nyaraka zilizoainishwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb)) maombi yatumwe kabla au saa **11:00** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), kabla au tarehe ya **28/10/2024**, kichwa cha barua pepe kitakuwa: **UTOAJI WA HUDUMA ZA UKANDARASI WA KUAJILI WAFANYAKAZI (MADEREVA) EOI-0000000635.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote ya kuonesha nia lazima ya andikwe kwa Kingereza.**

**Kumbuka:** Mradi wa EACOP utakagua na kutathmini hati zinazotumwa na kampuni zinazoonesha ili kupata orodha ya kampuni zilizokidhi vigezo vya awali. Kampuni zilizofuzu pekee ndizo zitapokea mwaliko, kwa makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA), mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuendeleza wa mchakato wa zabuni.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utekelezaji mfumo mpya elimu una umuhimu mkubwa kwa sasa

**KWA** miongo kadhaa, wadau wa elimu wamekuwa wakitoa maoni kwamba mfumo wa elimu ulioko nchini, hauendani na mazingira ya sasa ya sayansi na teknolojia pamoja na hali halisi ya maisha.

Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa ni kwamba mfumo huo umerithiwa kutoka ule wa kikoloni na kwa mazingira ya sasa haufanyi vijana wanaohitimu kuwa na maarifa mapana katika kukabiliana na changamoto za siku kwa siku katika maisha hasa kujitegemea.

Licha ya kudaiwa kuwa mfumo huo umerithiwa kutoka kwa mkoloni, baadhi ya wadau hao wamekuwa wakisema mabadiliko ya sera na falsafa kutoka uchumi hadi uliokuwa chini ya Ujamaa na Kujitegemea kwenda uchumi wa soko katika muktadha wa soko huria na utandawazi, yameathiri kwa kiasi kikubwa sekta hiyo.

Hoja kubwa wanayoitoa ni kwamba kuwapo kwa soko huru na kuruhusu sekta binafsi kuingia kwa nguvu zote katika sekta ya elimu, kumesababisha kuwapo kwa shule na vyuo vingi ambavyo falsafa yao ni kufaulisha watoto. Kwa maneno mengine, elimu imegeuzwa kuwa biashara, hivyo kinachozingatiwa hapo ni fedha na si ubora au kiwango cha elimu inayotolewa.

Kuondolewa kwa elimu ya kujitegemea ambayo ilikuwa inawafanya vijana kujifunza pia stadi za maisha kama vile mapishi, kilimo, mifugo, useremala na uashi, kunaelezwa kuwa ni moja ya sababu zilizofanya elimu kupungua thamani yake. Vijana wengi wanaomaliza hata chuo kikuu, hawana maarifa wala uwezo wa kufanya mambo ya kuwawezesha kupambana na changamoto katika maisha.

Aidha, sababu nyingine inayoelezwa kuwapo kwa hali hiyo ni mwanzoni mwa miaka ya 2000 wakati wa serikali ya awamu ya tatu. Katika kipindi hicho, alitokea Waziri ambaye kwa utashi wake aliamua kubadilisha mtaala uliofuta baadhi ya masomo yakiwamo ya sayansi na kilimo.


Hatua ya kuwapo kwa utitiri wa shule na vyuo bila kuwekwa mifumo thabiti ya uthibiti, imetajwa kuwa sababu kwa kuwapo kwa hali iliyoko katika sekta ya elimu. Vijana wengi wanahitimu vyuo na kukosa ajira kwa sababu serikali na sekta binafsi hazina uwezo wa kuajiri idadi yote hiyo ambayo ni takriban wanafunzi 400,000 kwa mwaka.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, serikali imeanzisha mtaala mpya ambao umejumuisha stadi za maisha na kupokewa na wadau wengi kwamba utasaidia kuboresha elimu na kuwawezesha baadhi ya vijana kujiajiri badala ya kusubiri ajira kwenye kampuni na ofisi za umma na binafsi. Kupitia mtaala huo, vijana wanaomaliza hata elimu ya juu, watafunzwa maarifa ya namna ya kujiajiri badala ya kutegemea ajira.

Katika baadhi ya nchi, kutokana na ukosefu wa nafasi za ajira, serikali zimechukua jukumu la kuhamasisha uanzishwaji wa stadi za maisha katika ngazi zote za elimu ili kuwawezesha vijana kubadilika kifikra kuwa anapomaliza masomo ajiajiri badala ya kuajiriwa. Kwenye nchi hizo kama vile Afrika Kusini, Nigeria, Ghana na Botswana, vijana wengi wanawezeshwa ndiyo maana kuna idadi kubwa ya mamilionea vijana wanaoibukia.

Serikali, kutokana na umuhimu wa mtaala unaoangazia vijana kujitegemea baada ya kuhitimu masomo, ni vyema ikaanza utekelezaji huo mara moja ili kuondokana au kupunguza ombwe la ajira lililoko nchini kwa sasa. Jambo hilo ni muhimu kwa sababu litawezesha kutengenezwa kwa ajira nyingi kupitia makundi ya vijana kujiajiri ambao nao wataajiri wengine, hivyo kupunguza tatizo la ajira.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Malalamiko Daftari la Kura, pagumu pasahihishwe

Na Beatrice Moses

**UBORESHAJI** wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ni mchakato muhimu ambao unaendelea kutekelezwa nchini kwa sasa, chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hata hivyo malalamiko kadhaa yamesikika hasa kutoka kwa baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani.

Wamelalamikia utaratibu wa uandikishaji wakidai kuwa wapo ambao wanaandikishwa kinyume na mfumo rasmi, ikiwamo uandikishwaji wasiotimiza umri wa miaka 18, pia wamekaririwa wakivitaja baadhi ya vituo ambavyo wamedai kuwa ni hewa.

Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ambaye mwenye dhamana na jambo hilo amejitokeza na kuwataka wenye malalamikio wayawasilishe kwenye wizara hiyo na ushahidi ili hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Naamini kwamba licha ya Waziri Mchengerwa kutoa rai hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi nayo haiwezi kufumbia macho malalamiko hayo kwa kuwa yanaelekea kuichafua hivyo itatoa ushirikiano unaostahili ili kuweka bayana hali ilivyo.

Kama kuna vielelezo vya malalamiko hayo ni vyema viwekwe wazi kwa kuwa hayaleti picha nzuri kwa wananchi, pia inasababisha wengine kuwa na hofu ya kwenda kujiandikisha.

Ni wazi kuwa wakati ni mali sasa mtu afunge safari kwenda kujiandikisha kumbe amejiandikisha kwenye kituo hewa kama kweli kipo, mwingine akisikia ni wazi anavunjika moyo wa kwenda huko, hali hii itasababisha mchakato huo kudorora.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hutumia watendaji mbalimbali wakati wa Uandikishaji na Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura. Watendaji hawa ni pamoja na waratibu wa uchaguzi wa mkoa, maofisa waandikishaji, maofisa waandikishaji wasaidizi, waandishi wasaidizi na mwendesha kifaa cha bayometriki.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 17 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Mwaka 2024, Chama cha Siasa chenye usajili wa kudumu kinaweza kumteua mtu mmoja katika kila kituo cha uandikishaji kuwa wakala wa uandikishaji wa wapigakura.

Wajibu au majukumu ya wakala wa uandikishaji, kufuatilia zoezi la uboreshaji na kutazama kama linazingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kushirikiana na waandishi wasaidizi, kutambua wakazi wa eneo hilo na kutoa taarifa juu ya watu wasio na sifa.

Pamoja na majukumu tajwa, wakala wa uboreshaji hawaruhusiwi kuingilia shughuli za uendeshaji wa zoezi la uboreshaji. Msimamizi wa kituo ndiye mwenye mamlaka ya mwisho juu ya nani anastahili kuandikishwa au kuboresha taarifa zake kwa mujibu wa sheria, kufanya kampeni za kisiasa katika kituo cha uandikishaji kuorodhesha majina ya watu wanaojiandikisha.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Elimu ya Mpigakura Wakati Wa Uchaguzi Mkuu Wa Mwaka 2020, Daftari la Kudumu la Wapigakura limeanzishwa chini ya Ibara ya 5(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Kifungu cha 15B(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Tangu kuanzishwa kwa Tume, Daftari la Kudumu la Wapigakura limetumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Kwa mujibu wa Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na mambo mengine inawajibika:- (i) Kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapigakura wapya waliotimiza umri wa kuandikishwa; na (ii) Kusimamia na kuratibu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura Kwa mujibu wa Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 10 (1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, sifa za mtu kuandikishwa kuwa Mpiga Kura ni:- (i) Awe Raia wa Tanzania; (ii) Awe ametimiza umri wa miaka 18; na (iii) Awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

Nashauri ni vyema madai au malalamiko hayo yawe na ushahidi lakini kama hayana ushahidi wahusika watakaobainika kuzusha wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria kwa kuwa ni wazi watakuwa na lengo baya la kuhujumu mchakato.

Maana pia kuna taarifa zinazoonyesha kuwa baadhi ya vyama vina ukata hivyo vimeshindwa kuweka mawakala wao kwenye vituo, kwa hiyo siyo vyema kuhujumu mchakato huu ambao ni mwelekeo wa kupata viongozi wa mitaa watakaosaidia katika kuongoza kutafuta uchumbuzi wa kero zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

HABARI KITAIFA

# SADC yaweka mikakati miundombinu ya nishati

**Na Grace Mwakalinga**

KATIKA jitihada za kukuza ushirikiano na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imeweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha miundombinu ya nishati katika kanda hiyo.

Mkutano wa 57 wa Kamati Kuu ya Bwawa la Umeme Kusini mwa Afrika (SAPP), uliofanyika jijini Dar es Salaam, ulijadili namna nchi wanachama zinavyoweza kushirikiana kuzalisha, kusafirisha, na kusambaza umeme kwa tija ili kupunguza gharama za nishati na kuboresha biashara ya umeme ndani ya kanda nzima.

Nchi wanachama wa SADC ambazo zimeshiriki mkutano huo zikiwamo Tanzania, Malawi, Zambia, Angola na Zimbabwe, zimeweka mikakati ya kuzalisha umeme wa kutosha, kuunganisha gridi za umeme za kikanda, na kutumia vyanzo mbadala vya nishati ya jua, upepo, na jotoardhi.

Mikakati hiyo inalenga kukabiliana na changamoto za upungufu wa umeme, gharama kubwa za usambazaji, na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri uzalishaji wa nishati.

Akizungumza katika mkutano huo wa Southern African Power Pool SAPP, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayesimamia Umeme na Nishati Jadidifu, Khatibu Kazungu alisema kuwa Tanzania imepiga hatua katika miradi ya uzalishaji umeme likiwamo Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa sasa linazalisha megawati 700 na litafikia megawati 900 baada ya upanuzi kukamilika. Vilevile, serikali imejipanga kuzalisha megawati 600 kupitia nishati ya jua na megawati 5,000 kutoka jotoardhi.

Alisema Serikali ya Tanzania imejipanga vyema kutekeleza mikakati ya uzalishaji na usambazaji wa umeme kwa kuimarisha vyanzo vya nishati vilivyopo na kuanzisha miradi mipya ya umeme wa jua, maji, na jotoardhi.

Aidha, alisema hatua hizo zinalenga sio tu kukidhi mahitaji ya ndani, bali pia kutoa fursa ya kuuza umeme kwa nchi jirani kama Zambia, ambayo kwa sasa inakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa umeme.

"Tanzania, ikiwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa miradi ya nishati mbadala na asilia, tunaahidi kuendelea kushirikiana na SADC katika kuimarisha miundombinu ya umeme, kuunganisha mikoa ya pembezoni kwenye Gridi ya Taifa, na kuwekeza katika miradi ya nishati safi kama vile jua na jotoardhi," alisema Kazungu.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Costa Rubagunya, alisema wanajikita katika miradi ya kuimarisha uzalishaji wa umeme kwa kushirikiana na mitandao ya kikanda kama vile Southern African Power Pool (SAPP).

Alisema kuwa kujiunga kwa Tanzania na mitandao ya umeme ya kikanda kutaongeza uwezo wa nchi kuuza umeme kwa nchi nyingine za SADC, hasa zile zinazokabiliwa na upungufu wa nishati.

Rubagunya alifafanua kuwa Tanzania itaendelea kuwekeza katika miradi ya umeme ili kuhakikisha taifa lina umeme wa kutosha kwa matumizi ya ndani na biashara ya kikanda.

Aidha, alisema miradi hiyo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania na pia kwa kusaidia nchi jirani zinazoathirika na upungufu wa nishati.

Mwenyekiti wa mkutano huo kutoka nchi ya Malawi, Steven Dihwa, alisisitiza kuwa ushirikiano wa kikanda katika masuala ya nishati ni muhimu ili nchi za SADC ziweze kupata umeme wa gharama nafuu na wa uhakika.

Alisema kuwa mikakati ya pamoja ya kuunganisha nchi wanachama kwenye gridi za umeme ni hatua kubwa kuelekea kufanikisha malengo ya maendeleo endelevu kwa kanda nzima.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Prof. William Palangyo (waliokaa kulia), akitiliana saini mkataba na Mwakilishi wa Kampuni ya Ujenzi ya Salem, Charles Casmir jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la taasisi hiyo mjini Singida. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali, Amsons zakubaliana kupanua soko la saruji

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imetia saini makubaliano na Kampuni za Amsons Group kuongeza uzalishaji wa saruji kutoka tani 1,000 za klinka hadi 10,000 kwa siku ili kupanua wigo wa biashara.

Lengo la makubaliano hayo ni kupanua soko la bidhaa hiyo hasa katika mikoa ya kusini na nchi jirani za Zambia, Malawi na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, alisema makubaliano hayo yanahusu ushirikiano wa kuongeza uzalishaji wa saruji katika kiwanda cha Saruji cha Mbeya kutoka tani 1,000 hadi 5,000.

Alisema pia watajenga kiwanda kipya cha saruji mkoani Tanga chenye uwezo wa kuzalisha tani 5,000 za klinka na kuongeza uzalishaji hadi tani 10,000.

Alisema wameamua kuongeza uzalishaji katika kiwanda cha Mbeya Cement baada ya soko lake kushuka kutokana na kutowekezwa kwa muda mrefu.

"Nafikiri kwa kufanya hivyo tutalikamata vizuri soko la Tanzania Kusini ambalo limekuwa letu asilimia 70 hadi 75 kwa muda mrefu, lakini pia inakuwa mwanzo kwa kwenda kusambaza kwenye soko la nchi jirani," alisema.

**"Nafikiri kwa kufanya hivyo tutalikamata vizuri soko la Tanzania Kusini ambalo limekuwa letu asilimia 70 hadi 75 kwa muda mrefu, lakini pia inakuwa mwanzo kwa kwenda kusambaza kwenye soko la nchi**

Alisema kumekuwa na uzalishaji mkubwa wa saruji nchini kutokana na uhitaji wa bidhaa hiyo kuwa kubwa hali inayochochewa na ongezeko la watu.

"Matumizi ya saruji tunayaona kwenye miundombinu, ujenzi wa nyumba, kwa sababu pia idadi ya Watanzania inakuwa kwa kasi," alisema.

Alisema uzalishaji huo utachagiza kuongezeka kwa kodi nchini, sehemu ya mabadiliko ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anataka ayaone katika ofisi ya Msajili wa Hazina.

Alisema uwekezaji huo ni sehemu ya mwitikio wa mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo serikali imekuwa ikiyajenga.

Mkurugenzi wa Fedha wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ahmed Mhada alisema, uwekezaji Kiwanda cha Mbeya Cement utagharimu Dola za Kimarekani milioni 130 na kiwanda cha Tanga Dola za Kimarekani milioni 190 jumla ikiwa ni Dola milioni 320.

Alisema uwekezaji huo unategemewa kuzalisha jumla ya ajira 12,000 na kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

"Ukiangalia hapo kodi za serikali zitaendelea kukusanywa za kutosha, na mauzo kufika zaidi ya tani milioni 4.2 kutokana na uwekezaji huu," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mbeya Cement, Siasa Mzenzi, aliishukuru serikali na kampuni ya Amsoms kwa uwekezaji huo na kuwahakikishia kuwa atakuwa tayari kusimamia uwekezaji huo kwa manufaa ya kiwanda hicho na jamii kwa ujumla.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



## Wajane washauriwa kutatua kesi kisheria

**Na Halfan Chusi**

MKURUGENZI mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen Kijo-Bisimba, amewashauri wajane nchini kutumia mifumo ya kisheria kutatua kesi za mirathi na umiliki ardhi badala ya kuwatumia viongozi wa kisiasa.

Akizungumza katika mkutano wa wajane jijini Dar es Salaam uliowakutanisha zaidi ya 300 kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuandaliwa na Taasisi ya Newlife in Christ alisema ni rahisi kupoteza haki zao iwapo hawatatumia mifumo ya kisheria.

"Hizi kesi hasa za masuala ya ardhi baadhi mnapenda kuzipeleka kwa wanasiasa na wao pia wanazipenda kweli, lakini wengine wanapoteza muda na baadaye kesi inarudi tena mahakamani.

"Kesi ya ardhi inatakiwa kutatuliwa kwa wakati mwafaka tatizo linapojitokeza, usipopeleka mapema halafu uje kuipeleka imepita miaka 12 au zaidi kesi inakuwa imekufa kwahiyo hutaipata haki yako," alisema Dk. Hellen.

Akijibu maswali kutoka kwa wajane hao Hellen Kijo ambaye kitaaluma ni mwanasheria aliwaeleza jinsi alivyokutana na kesi za aina hiyo ambazo nyingine zilifika kwa kuchelewa hali iliyopelekea wengine kupoteza haki zao za kumiliki ardhi.

Mbali na suala hilo la umiliki ardhi kwa wajane na Dk. Hellen aliwaeleza umuhimu wa kuzifahamu sheria tatu zinazoweza kutumika katika masuala ya ugawaji mali za marehemu na mambo ya kuzingatia wanapoishi na wenzi wao wakiwa hai, ikiwamo kuhakikisha mali wanazochuma pamoja zinaandikwa kwa majina ya pande mbili, wa mwanamume na mwanamke.

"Sisi wanawake tuna roho nzuri sana unakuta kiwanja mmenunua pamoja, lakini kwenye hati unasema andika tu jina la mwanamume sasa hiyo huwa inaleta matatizo baadaye kwa kuwa mali zinaonekana zote ni za kwake," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Newlife in Christ, Dk. Ally Mmanyi aliwashauri wajane hao kumtumainia Mungu katika matatizo yao kwa kuwa ndiye mfariji wa kweli.

"Sote tutakufa tu siku moja wala hakuna anayeweza kulazimisha kuishi duniani muda wake ukiwa umeisha au kulazimisha kufa kabla ya wakati ukifanya hivyo wewe ni jehanamu moja kwa moja," alisema.

Alisema kuwa wajane wengine wamekuwa wakifadhaika mioyoni lakini wanapaswa kutambua hatua hiyo ni ya lazima kwa kuwa ndiyo mfumo wa maisha uliopangwa na Mungu mwenyewe huku akiwasihi kutokata ya maisha.

Alisema upo umuhimu mkubwa kwa wajane kukutana angalau mara moja kwa mwaka katika kila mkoa, ili kutiana moyo na kupeana mbinu za maisha.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, tuzo ya Usimamizi na Uratibu wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi nchini, kwenye uwanja wa EPZ Bombambili, mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aikabidhi tuzo NSSF usimamizi, uratibu hifadhi ya jamii sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeshinda tuzo ya Usimamizi na Uratibu wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi nchini, wakati wa kilele cha Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika kwenye uwanja wa EPZ Bombambili, mkoani Geita.

Tuzo hiyo imetolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kupokewa na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, wakati wa ufungaji wa maonesho hayo.

Aidha, NSSF imeshinda tuzo ya mshindi wa kwanza katika kundi la Hifadhi ya Jamii na Huduma za Bima zilizotolewa Oktoba 12, 2024 na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, wakati wa maonesho hayo.

Mshomba alisema utoaji wa huduma kidijitali umekuwa nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma za NSSF zinawafikia wanachama popote walipo, ikiwamo kufungua madai ya kuomba mafao mbalimbali.

Aliwataka waajiri wa sekta binafsi kusajili wafanyakazi wao NSSF pamoja na kuwasilisha michango kwa wakati, kwa kuwa hilo ni takwa la sheria na vilevile kuwezesha Mfuko kuendelea kukua na kutoa huduma bora.

Aidha, Mshomba alitoa rai kwa watu waliojiajiri katika sekta isiyo rasmi wakiwamo wachimbaji wadogo wa madini, mamalishe, babalishe, bodaboda, wavuvi, wakulima, wafugaji na wajasiriamali mbalimbali kujiunga na kuchangia NSSF kwa sababu ndiyo njia sahihi ya kupunguza umasikini wa kipato na kujikinga dhidi ya majanga mbalimbali.

**Aidha, NSSF imeshinda tuzo ya mshindi wa kwanza katika kundi la Hifadhi ya Jamii na Huduma za Bima zilizotolewa Oktoba 12, 2024 na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, wakati wa maonesho...**

Naye Mkurugenzi wa Uendeshaji, Omary Mziya, amesema mfuko utaendelea kutoa huduma bora kwa wanachama kupitia mifumo ya TEHAMA na hivi sasa wanachama wanaweza kufungua madai yao kwa njia ya kidijitali bila ya kulazimika kufika katika ofisi za NSSF.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema kupitia maonesho hayo Mfuko ulifikisha elimu ya hifadhi ya jamii kwa makundi mbalimbali yakiwamo ya wachimbaji wadogo wa madini pamoja na wajasiriamali zaidi ya 1,500 wilayani Bukombe. "Maonesho ya madini yalikuwa fursa kwa NSSF kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii, kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta isiyo rasmi, tutoe elimu kuhusu huduma za kidijitali pamoja na fursa za nyumba na viwanja," alisema Lulu.

Awali, Meneja wa NSSF Mkoa wa Geita, Winniel Lusingu alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Mkoa huo imeweka lengo la kukusanya Sh. bilioni 104 na kuwa mwaka wa fedha uliomalizika walikusanya Sh. bilioni 64. Alishukuru ushirikiano mkubwa wanaopata kutoka kwa uongozi wa mkoa huo, waajiri, menejimenti na wafanyakazi wote wa NSSF.

# TCRA yaelimisha wadau mipango kusimamia taka za Ki-elektroniki

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, amesema hatua zilizochukuliwa na Tanzania kuanzia mwaka jana kuhusu utupaji salama wa taka za kielektroniki ili kulinda afya za watu na mazingira zimekuwa na manufaa.

Akizungumza juzi na wawakilishi wa Chama cha Wafanyabiashara wa Kariakoo kwenye kikao cha mashauriano jijini Dar es Salaam, alisema ukaguzi wa awali na ukusanyaji wa ada ya mazingira kuanzia Mei 2023 unalenga kusimamia utupaji wa vifaa vya mawasiliano vilivyofikia mwisho wa matumizi kwa usalama bila kudhuru afya na mazingira.

Alisema Kariakoo ni kitovu cha biashara za vifaa vya waagizaji na watumiaji huduma za mawasiliano ya ki elektroniki na kwamba ni muhimu wajue utaratibu wa kuteketeza takataka hizo.

Dk. Bakari aliwaeleza wafanyabiashara hao hatua zilizochukuliwa na TCRA kuwa ni kusimamia taka za kielektroniki chini ya kanuni za mwaka 2020 kuhusu Viwango vya Vifaa na Usimamizi wa Taka Elektroniki.

"Tanzania inasimamia utupaji wa taka elektroniki. Inahimiza utupaji sahihi na salama ili kuzuia vijenzi hatarishi na vyenye sumu vilivyomo kwenye vifaa vya mawasiliano visiathiri afya ya binadamu na mazingira," alisema.

Alisema ada ya mazingira ilianzishwa kuwezesha usimamizi wa utupaji taka zitokanazo na vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki.

Eco Levy inawapa watengenezaji uwajibikaji wa kuhakikisha vifaa vyao vinatupwa kwa usahihi. Na kwamba vifaa vyote vya mawasiliano vinavyoingia Tanzania vinakaguliwa kwenye nchi vinakotoka.

Alisema vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingia Tanzania vinatakiwa kuidhinishwa na TCRA, na kwamba mamlaka inatoa leseni za uagizaji na usambazaji wa vifaa vya mawasiliano.

"Kanuni za mwaka 2021 za usimamizi wa vifaa vya umeme na elektroniki zinawataka waagizaji wa vifaa hivyo kulipa ada ya mazingira kabla havijasafirishwa kuja Tanzania," alisema."Kanuni hizo zinahusu hatua zote za vifaa vilivyoagizwa. Hizi ni pamoja na uagizaji, usambazaji, uuzaji, uchakataji, ukarabati, uundaji, ufumuaji na utupaji wa taka za vifaa vya umeme na vya kielektroniki Tanzania," alisema.

Aidha, Tanzania inafuata kanuni na misingi ya kimataifa katika usimamizi wa taka elektroniki.

Alisema usajili na ukaguzi wa vifaa vya mawasiliano kwenye nchi vinakotoka unazingatia masharti ya Mkataba wa Basel kuhusu usafirishaji wa taka hatarishi nje ya mipaka ya nchi na utupaji wa taka hizo, baada ya matumizi yake kufikia kikomo.

Mkutano wa TCRA na wawasilishi wa wafanyabiashara Kariakoo ni sehemu ya kampeni ya Mamlaka ya kuongeza uelewa wa wadau kuhusu utupaji salama wa taka elektroniki.

# MATAGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: ACCOUNTS PAYABLE**
**Job Type:** Full Time
**Reports to:** CHIEF ACCOUNTANT
**Location:** Dar es Salaam (TZ)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

The Accounts Payable is based in Dar es Salaam.
More than 900 invoices and expense claims monthly.
EACOP Ltd is a company registered in the UK, domiciled in UG with a permanent establishment in TZ; it has 4 shareholders, TotalEnergies, UNOC, TPDC and UNOC. It is to build and operate a 1442 km oil pipeline from Hoima (UG) to Tanga (TZ)

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Receive invoices from vendors, control that they meet the requirements, post the receipt and submit for approval.
- Liaise with Tax team for follow up of VAT relief utilization process.
- Liaise with other departments, Cost controllers and Contract & Procurement department for invoice approval, purchase orders & call offs creation/ release, goods/service receipts; sort out issues.
- Liaise and respond to vendors and internal inquiries.
- Reconcile monthly supplier statements, identify discrepancies and make corrections where necessary.
- Assist the Chief Accountant during external audits (statutory and financial, fiscal, shareholders, national authorities)

### CONTEXT AND ENVIRONMENT

- EACOP Ltd is fully engaged with the construction of the pipeline.

### ACCOUNTABILITIES

- Timely processing and posting of vendor invoices for payment.
- Follow up of vendors' accounts.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**
- Bachelor in Accounting, Finance or Business administration – ACCA Level 2.
- Knowledge of Workday or similar ERP, Microsoft Office Suite.

**Experience Required:**
- Minimum 3 year experience within an Accounting Department.

**Abilities:**
- Organizational, team spirit and interpersonal skills.
- Excellent level in English (spoken & written)

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: ELECTRICAL ENGINEER**
**Job Type:** Full Time 5 days/week and on duty period
**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and Inspection, N+ 2: Operations Director for TZ
**Location:** MST – Tanga with frequent travel to EACOP pumping station site.

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

The Electrical Engineer will support the Site Electrical Technicians for electrical activities. The Electrical Engineer who will be located at MST will be under authority of the Maintenance Inspection Head, one located at Kampala back office under Maintenance Engineer. Electrical Engineer will oversee the electrical maintenance activities of PS1 perimeter for one base at Kampala, and TZ station for one based at MST. According to this perimeter they will manage technicians, service contracts and interfaces with power grid stations or providers.
He / she will oversee managing several service contracts such as UPS, Lighting, HVAC, vendors maintenance services.
He/she is responsible for maintenance and inspection activities of EACOP electrical equipment that are mainly:

- Pump package driven by electric VFD motor up to 2 M Watts.
- HT power distribution system.
- PV farm.
- BESS (Battery system.)
- UPS.
- Electrical Control Panels, MCC, Switchgears, PLC's, VFD's, MoV's, & CB's,
- Diesel generators (4 M Watts.)
- MVs, HV & LV Systems.
- Hydraulic systems (loading arms, Gangway, accumulator, etc.)
- Actuated valves up to 30" diameters.
- Building electrical wiring system and lighting system.
- Air Compressors.
- Nitrogen Generator.
- Fire Heater, Heat Exchanger, Electric Heater.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**Production Operations:**
- To ensure the performance / availability of the facilities, highlight miss-functions, compile relevant data, establish a diagnosis, produce corresponding report with corrective actions and participate in the implementation of the agreed plan.
- Prepares periodic or specific reporting of the maintenance activities under his/her responsibilities.
- Preparation/reviews of the complex or with external electric power provider interface PTW dossiers and confirm completeness.
- Preparation of Procedures for operation and shutdown instructions.
- Participation in production incidents or shutdowns are properly investigated and sign the associated production reports.
- Assists in identification of possible areas of optimization, potential improvement to increase equipment availability and cost reduction.
- Ensures execution of both planned and unplanned maintenances of electrical equipment so that to ensure optimization of equipment efficiency and availability.
- Assists in the evaluation and participate on the validation of the Site Modification Request (SMR/RFM); consolidate the technical dossier on maintenance side.
- Participates in validation of the commissioning / pre-commissioning of new equipment or equipment modified; ensure the good management of the punch list after the hand-over.

**Maintenance Operations:**
- Participates on budget / Work program preparation for light and heavy maintenance.
- Participates and assists in the preparation of annual maintenance shutdown activities plan.

**Quality Assurance:**
- Assists in supervising and evaluating the performance of the Maintenance service contractor, secure that REXs are well implemented for the maintenance plan to be updated.
- Site Management:
- Builds TEAM environment for MST perimeter.
- Evaluates the personnel working in his team and make proposals for their training plan.
- Defines team member objectives.
- Contributes to the training of all personnel under his/ her responsibility.
- Organizes Job Training (OJT) in coordination with the Training Department.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**
- Bachelor's degree in electrical engineering or similar.
- Proficiency in Oral and written English.
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System.)
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**
- 10 years of experience in Oil & Gas industry, electric power service or a high potential, 3 years minimum as site discipline or multidiscipline leader or supervisor.
- MS office good experience.
- Primavera uses good experience will be added advantage.
- Other skills required: responsibility, natural authority, decision making, good communication skills, organization, and methods.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**





EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**VACANCY ANNOUNCEMENT**

**Job Title: FABRICATION, MAINTENANCE & CAMPAIGN ENGINEER**

**Job Type:** Full Time – and duty period to consider.

**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and Inspection, N+ 2: Field Operations Manager

**Location:** MST – Tanga – regular travel to EACOP site to consider.

**WHO WE ARE**

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

**JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION**

- As Campaign Engineer for EACOP, you will manage campaign activities in 4 perimeters. This means you will be able to shape and develop a central role with great influence in safe, timely and effective execution of campaign activities. This is with the possibility to continuously use and develop your competencies in ensuring the quality and effectiveness of Campaign activity reporting, sub-contractor efficiency and work preparation on future campaign activities.
- You will get to use your knowledge and experience applying a range of techniques when developing the Campaign Model taking into consideration the local market conditions, partial or full field shutdown opportunities, the mono or multi métier various possible technical approaches, the various resources available or to develop etc.
- As Fabric Maintenance Engineer, you will manage fabric maintenance contractor who will provide various services as scaffolding, insulation removal and installation, piping repair, routine painting, cleaning, assistance to operation, rope access, civil works.
- Interface regarding activity planification and with other entities.

**DUTIES & RESPONSIBILITIES**

- Contributes to HSE performance in line with EACOP objectives.
- Integrates into an execution plan the "campaign-able" activities prepared by Maintenance, Inspection Services, Engineering & Construction.
- Ensures the Work Packs, Procedures, Permits to Works, Risk Assessments and Toolbox Talks are correctly drafted by the Support Entities.
- Ensures the main resources of the scopes are provided in time by the Support Entities.
- Ensures the Isolations, Inhibitions, Flushing, Inerting various scopes are provided.
- Provides input for the Campaign various Planning and Scheduling
- Provides and Execution Plan and source the supporting resources (e.g., vessels, scaffolding, HSE supervision)
- Prepares and executes the on boarding process of the various workforces prior to the execution phases to commence.
- Executes the Campaign safely and efficiently.
- Manages related service contracts to improve campaign efficiency.
- Contributes to the 2-Year visions of planned campaigns and the 90-day planning.
- Influences the 90-day planning.
- Influences the 5-week planning.
- Issues T-REX.

**HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES**

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

**QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED**

**Academic Qualifications:**

- Bachelor level or similar.
- Proficiency in oral and written English.
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System.)
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- 10-15 years of experience in Oil & Gas industry or a high potential
- Site -multi sites and multidiscipline planning preparation or activity management experience.
- Maintenance Contract management.
- Full field/Industrial site shut down experience.
- Primavera good experience.

**HOW TO APPLY**

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

# Rugambwa ahamasisha wananchi kujiandikisha uchaguzi mitaa

**Na Waandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu Mwandamizi wa Katoliki Jimbo Kuu Tabora, Kardinali Protase Rugambwa amewataka wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari la mkazi ili wapate fursa ya kushiriki kuchagua viongozi bora katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini mwezi ujao.

Kardinali Rugambwa alitoa wito huo juzi wakati akiwaongoza mamia ya wakazi wa Manispaa ya Tabora kujiandikisha katika daftari hilo ili watumie haki yao ya msingi kuchagua wenyeviti wa mitaa, kijiji na kitongoji katika uchaguzi huo utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu na kuondoa mlalamiko miongoni mwao.

"Naomba na wengine waendelee kujiandikisha ili kuchagua viongozi watakaotusaidia kuleta maendeleo na kudumisha amani, furaha na haki tunazoziitaji, tusibaki kupiga tu kelele au kulalamika bali tulalamike lakini tukiwa tunawajibika," alisema Kardinali Rugambwa.

**Ofisa Uchaguzi Ngara, James John, alisema wanatarajia kuandikisha watu 138,021 katika vituo 423 vilivyotengwa wilayani humo na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi**

Katika hatua nyingine; Mkuu Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, Kanali Mathias Julius, licha ya kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kujiandikisha katika daftari hilo, amepiga marufuku raia kutoka nje ya nchi kushiriki mchakato huo vinginevyo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Ofisa Uchaguzi Ngara, James John, alisema wanatarajia kuandikisha watu 138,021 katika vituo 423 vilivyotengwa wilayani humo na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kutimiza haki yao kikatiba.

Diwani wa Kata ya Sirari Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Amos Sagara, alisema mawakala wameelekezwa kuhakiki uraia wa watu wanaojitokeza kujiandikisha kwa kuwaomba Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na barua za utambulisho kutoka mamlaka za vijiji na mitaa wanayotoka.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kanisani cha kata hiyo, Ngogo Kisike alisema wanatoa elimu kwa wananchi ili kuwasaidia kutofautisha kati ya daftari la kudumu la mpiga kura na hilo la wakazi kwa ajili ya uchaguzi huo wa serikali za mitaa.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Tarime, mkoani humo, Noverty Kibaji aliwaonya wasimamizi wa uchaguzi huo kuepuka kuandikisha raia wa nje.

Alisema baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakivuka na kuingia nchini kupitia mpaka wa Sirari unaopakana na Tanzania na Kenya na kushiriki mchakato huo kinyume.

Alisema wametoa taarifa ofisi ya Idara ya Uhamiaji katika mji wa Sirari kwa ajili ya kufanya uchunguzi na kuchukua hatua.

Baadhi ya wakazi wa Tarime, akiwamo Bashiri Abdalah waliwaomba viongozi wa mitaa, vijiji na kata kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kushiriki mchakato huo.

**Imeandikwa na Vitus Audax**

# Vijana walilia ajira mgodini

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya vijana wanaoishi maeneo yanayozunguka mgodi wa dhahabu wa Barrick North Mara wameomba kupewa kipaumbele katika ajira mgodini hapo ili waondokane na taa ya kuvamia mgodini 'intruda' ili kujipatia kipato.

Vijana hao, akiwamo Yohana Mwita, Mkazi wa Matongo walitoa ombi hilo ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira na kulazimika kuvamia mgodi huo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kenyange, Hadija Sanga, licha ya kushukuru mgodi huo kwa kuwajengea shule mpya ya kisasa, aliuomba uweke umeme, maji na serikali kutoa ajira kwa walimu hususani wa Kingereza.

Akijibu maombi hayo wakati wa ziara ya waandishi wa habari mgodini hapo, Meneja wa Mgodi huo, Apolnary Lyambiko, alisema kwa nyakati tofauti wametoa ajira kwa wazawa zaidi ya 4,000 sawa na asilimia 51 wa fani mbalimbali.

Lyambiko, alisema kati ya hao, wameajiri walinzi 560 kutoka vijiji 11 vinavyozunguka mgodi huo.

Akizungumzia miradi ya maendeleo, alisema wametekeleza zaidi ya 115 katika sekta ya elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara.

miradi hiyo, wameikabidhi halmashauri shule ya Kenyangi ambayo ujenzi wake umegharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.2 ikiwa na madarasa 12 na nyumba mbili za walimu.

Katika hatua nyingine; Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Dk. Mark Bristow, amewakabidhi wananchi shule ya msingi ya kisasa iliyojengwa katika Kijiji cha Matongo kwa ufadhili wa mgodi huo na kueleza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya ushirikiano na jamii na serikali ambaye ni mbia wake kupitia Kampuni ya Twiga Minerals.

Bristow, alisema ujenzi wa shule hiyo umegharimu zaidi ya Sh.milioni 400 baada ya makubaliano na jamii ya eneo hilo ya kuhamisha shule ya msingi iliyokuwa karibu na eneo la uzalishaji ili kupisha upanuzi wa shughuli za mgodi huo.

**Imeandaliwa na Timothy Itembe, Samson Chacha, Ada Ouko na Ambrose Wantaigwa (TARIME)**

ama
ALHAMISI OKTOBA 17, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




SIKU YA KUNAWA MIKONO DUNIANI

**Uelewa 'bado sana' namna kutakatisha, mwafaka haujafikiwa mbinu za kukausha**




Daktari ataja magumu ya utoaji mimba holela, mwanasheria ana adhabu yake




**Ijue PID; ugonjwa unaomtesa mama, lakini wanaouelewa vilivyo wachache**

SIKU YA KUTOKOMEZA UMASKINI DUNIANI

# Safari ya TASAF kutekeleza maelekezo ya Rais kupunguza vifo kupitia MMAM

**Na Faustine Feliciane**

MNAMO Septemba mwaka 2021, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa, Humphrey Polepole, alimwelekezea pongezi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na serikali yake, kupunguza umaskini kwa wananchi wake.

Polepole, ambaye nafasi yake ilikuwa na dhamana na Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) akanena: "Uamuzi huo unaonyesha nia ya dhati ya serikali kuzikwamua kaya zinazoishi katika mazingira maskini..."

Awali katika tukio hilo, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, akasema: "Serikali imetenga fedha za kutosha kuzifikia kaya zote zenye uhitaji."

Akaendelea: "Toeni taarifa kama kuna kaya zilizosahaulika ili watendaji wetu wazifikie na kukamilisha taratibu za uandikishaji na serikali itahakikisha kila Mtanzania anayestahili kunufaika na mpango huu, anapata ruzuku."

Mwaka mmoja baadaye, Novemba 2022, Rais Dk. Samia akatangaza kuongeza muda kwa wanufaika wa Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) hadi mwaka ujao, 2025, kauli iliyopokewa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora wakati huo, Deo Ndejembi, kwa mtazamo chanya kuwa:

"Nimshukuru Rais Samia kwa upendo aliouonyesha kutuongezea muda wa mradi huu... Hili ni jambo kubwa ambalo hakika Rais wetu amelifanya kwa wanufaika wa TASAF."



Jengo la watumishi wa Kituo cha Afya, kilometa 10 nje ya Arusha, lililojengwa na TASAF. **PICHA ZOTE: MAKTABA**



Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray.

**KILELE MAFANIKIO**

Sasa ni miaka miwili tangu nyongeza ya muda wa TASAF iliyoelekezwa na Rais Dk. Samia, huku dunia ikiadhimisha 'Siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani,' nchini TASAF ikiwa imebebeshwa dhamana kwa Mkurugenzi Mkuu, Shedrack Mziray.

Ana ufafanuzi kuwa mfuko huo umeendelea kubeba dhamana hiyo ya kiserikali kitaifa, ikijenga na kukarabati vituo mbalimbali vya afya katika maeneo ya vijijini pamoja na kusaidia upatikanaji bima za afya kwa kaya maskini.

Mziray ana ufafanuzi kwamba mfuko huo kwa kushirikiana na wadau, pia halmashauri mbalimbali nchini, wamesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua kwa kujenga vituo vya afya vya kisasa, hali inayoendana an utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

"Kwa baadhi ya maeneo hasa vijijini, ambako hasa TASAF tunalenga kusaidia kaya zisizojiweza, kumekuwa na changamoto kubwa ya huduma za afya. Kwa kushirikiana na halmashauri na serikali za mikoa, tumekuwa tukiboresha miundombinu," anasema Mziray.

Hapo anatumia mfano katika Kijiji cha Themi, Kata ya Bwawani umbali wa kilometa zaidi ya 50 kutoka Arusha mjini, hakikuwa na kituo cha afya, hali iliyowalazimu wananchi wa kijiji hicho kutembea umbali zaidi ya kilometa 10, kwenda Kata ya Mbuluma ambako kuna kituo cha afya.

"Kumekuwa na changamoto ya miaka mingi hasa kwa kinamama wajawazito kwenye kijiji hicho. Inawalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, lakini kwa sasa kuna ahueni kidogo," anasema Mziray.

Pia ana maelezo kuwa wamewezesha ujenzi wa majengo manne muhimu katika kituo hicho cha afya kijijini hapo, ambacho kina Idara ya Wagonjwa wa Nje (OPD), maabara, vifaa vya uzazi ikiwamo chumba cha upasuaji (OT) na jengo la watumishi.

"Kituo hiki cha afya kinaweza kuhudumia zaidi ya watu 20,000 (kwa mwaka), hasa kwa vile kinapakana na wilaya ya Simanjiro. Uwapoo wake, utasaidia sana kupunguza changamoto walizokuwa wakizipata wagonjwa hususani 'wamama' wajawazito, kwa sasa watakuwa na sehemu sahihi na salama ya kujifungua," anaeleza Mziray.

**RUZUKU YA OPEC**

Anafafanua kuwa uwekezaji huo mkubwa kwenye sekta ya afya katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, ni sehemu ya ruzuku ya Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OPEC) ya dola milioni 50 (sawa na Sh. bilioni 131.68) iliyotolewa kwa Tanzania kupitia TASAF.

Ni aina ya uwekezaji unaolenga

INAENDELEA UK.12

AFYA

## SIKU YA KUNAWA MIKONO DUNIANI

# Uelewa 'bado sana' namna kutakatisha, mwafaka haujafikiwa mbinu za kukausha

**Na Christina Mwakangale**

KILA siku ya Oktoba 15 ya mwaka (Juni Jumanne), huwa ni maalumu Siku ya Kunawa Mikono Duniani.

Lengo ni mapambano dhidi ya wadudu wenye madhara kwa binadamu kupitia mikono, kutokana na kuwa chanzo cha kushika vitu mbalimbali.

Mbinu rahisi na inayokamilisha unawaji halisi ni kutumia sekunde zisizopungua 20. Wataalamu wa afya wanashauri wimbo wa "happy birthday to you…' uimbwe mara mbili, kuzikamilisha sekunde hizo unaponawa ukiwa mbele ya sinki au beseni lako la maji tiririka popote.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linahimiza unawaji mikono kwenye jamii baada ya mtu kutoka chooni, kupiga chafya, kabla ya kuandaa chakula na matunda, baada ya kumhudumia mgonjwa au kumtawaza mtoto.

Kadhalika, mikono inatajwa iwe safi baada ya mtu kutoka kwenye maeneo ya mkusanyiko mkubwa wa watu, kushika vitasa vya milango ya gari, chuma daladala, nyumba na hata fedha, kwa sababu hizo ni sehemu mojawapo za kutunza vijidudu.

Katika kuidhamisha siku hiyo, Wizara ya Afya, imetoa maelekezo yapatayo nane, ikiwamo hatua za kufuata baada ya kunawa yaani kukausha maji mikono.

Juzi katika ukurasa wake wa maadhimisho hayo, mbali na kueleza hatua za unawaji mikono ambao lazima uambatane na sabuni na maji safi tiririka, WHO inashauri mikono ikaushwe kwa kuelekeza juu.

Kadhalika tovuti za masuala ya afya pamoja na WHO, Cleveland



Mtu akinawa mikono. **PICHA: MAKTABA**

Clinic na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC), inaeleza hali ya 'kukubaliana kutokubaliana' kwa wataalamu wa afya katika namna sahihi ya kukausha mikono baada ya kunawa.

WHO, inasema asilimia 34 ya maeneo ya kutoa huduma za afya barani Afrika, hayana maeneo rasmi kufanikisha unawaji mikono.

Mjadala na utafiti pia haujawahi kuwa na uwiano sawa, kwamba mikono baada ya kunawa, litumike taulo kila mmoja lake katika kujifuta au ikauke yenyewe!

Au sahihi ni mbadala, itumike karatasi laini (tishu/toilet paper).

Ingawa teknolojia imekuwa, mikono hufutwa kwa mashine ya kukausha mikono katika baadhi ya sehemu.

Tovuti ya kliniki hiyo inashauri pia, mikono unawaji wake usitumie maji ya moto, ingawa katika maeneo mengi dhana imejengeka kwamba unawaji aina hiyo huua vijidudu zaidi!

### HALI HALISI ILIVYO

Miongoni mwa makundi yanayoathiriwa na kutokunawa mikono ni watoto. Takribani watoto milioni 1.8 walio chini ya miaka mitano wanafariki dunia kila mwaka, kutokana na sababu kuu mbili na magonjwa yanayoua zaidi kundi hili, nimonia na kuhara, WHO.

Kwa mujibu wa tovuti ya USA CDC, kunawa mikono inaweza kutunza afya na kuepuka kusambaa kwa magonjwa hasa ya mfumo wa upumuaji na kuhara.

Vijidudu husambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kutoka ukutani, ardhini pale watu wanapozigusa sehemu hizo, lakini pia kwa kugusa macho, pia mdomo kisha mikono hiyo ikaenda kushika mlo au kinywaji na kula.

Kadhalika, unawaji mikono upo wa aina tofauti na sekunde zake. Unaponawa kwa kutimiza hali ya usafi binafsi zisipungue sekunde 20; unawaji kwa wataalamu wa upasuaji na wauguzi sekunde ni zaidi ya 30. Hivyo, muda wa unawaji hutegemea kazi mtu anayofanya.

Kwa watoa huduma kwa wagonjwa WHO, inashauri upakaji rangi mikono wala kucha bandia kutohitajika, kwa sababu itazuia usafi wa mikono. Muda wote kucha ziwe fupi.

WHO, inasema watoto wafundishwe zaidi kunawa mikono na jamii iwe na taarifa mbalimbali katika zinazohusu kunawa mikono katika vyanzo kama mitandao ya kijamii, simu na televisheni.

Shirika hilo kimataifa linasema unawaji mikono hupunguza kiwango cha wagonjwa wa kuhara kwa kiwango cha asilimia 23 hadi 40, pia ina saidia kupunguza utoro shuleni kutokana ana magonjwa ya matumbo kwa asilimia 29 hadi 57.

Lingine ni kwamba, kunawa mikono kunapunguza magonjwa ya mfumo wa kupumua, kwa watu takribani asilimia 16 hadi 21.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), pia inasisitiza kunawa mikono kunamlinda/kumnusuru mtoto mmoja katika kila watoto watatu wanaougua kuhara; mmoja kati ya watano wanaougua nimonia. Pia, inaelezwa unawaji huo hupunguza matumizi ya dawa aina ya antibaiotiki.

WHO inasema ingawa wengi hunawa mikono, walio katika dhamira halisi ya kunawa, ambayo ni kusaidia kuondoa vijidudu. Inakadiriwa viwango vya unawaji mikono kwa mahitaji halisi ni kidogo kisichozidi asilimia 19.

## Safari ya TASAF kutekeleza maelekezo ya Rais kupunguza vifo kupitia MMAM

INATOKA UK.11

kufadhili mradi mkubwa unaofahamika kama 'Mradi wa Nne wa Kupunguza Umaskini Tanzania.'

Mpango huo unalenga kuimarisha miundombinu ya afya vijijini katika mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu na Arusha.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Mfuko huo, Japhet Boaz, anasema kaya maskini zanufaika na bima za afya, akieleza namna mfuko huo unavyowezesha kaya maskini kupata bima za afya na wepesi katika upatikanaji huduma hizo.

"Lengo la mfuko ni kupunguza kama sio kuondoa kabisa umaskini kwa kaya mbalimbali. Tunaamini afya bora ni mtaji wa kwanza kufikia maendeleo, tunasaidia upatikanaji wa bima za afya," anasema Boaz.

Mkurugenzi wa Huduma kwa Jamii, John Stephen, anasema walengwa pia wamekuwa wakishiriki katika programu mbalimbali za kuwaongezea kipato waweze kumudu gharama za maisha.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo wa huduma za jamii, programu hizo zinaiwezesha jamii kutoa fursa za ajira kwa kaya zinazofaidika, kuzalisha mapato ya ziada kwa matumizi bora na kupunguza athari za ugumu wa maisha.

"Mpango huu unaipa kipaumbele miradi midogo yenye mahitaji makubwa ya kazi, kwa kutumia asilimia 75 ya wafanyakazi wasio na ujuzi na asilimia 25 ya wanufaika wenye ujuzi," anasema Stephen.

### WANUFAIKA NA YAO

Mmoja wa wanufaika wa mfuko huo, Kashinde Issa, mkazi wa Mtaa wa Mbugani katika Manispaa ya Tabora, ambaye ni mama wa watoto saba, anasema alipandikishwa kwenye mpango huo, alikuwa ni mjasiriamali wa kuuza matunda, ambayo haikukidhi mahitaji ya familia yake, ikiwamo matibabu pale wanapougua.

Anasema tangu alipojiunga na mpango huo na kuanza kupata ruzuku, akaweza kubadili biashara na kuanza kuuza nguo za mitumba, hata baadaye akajenga nyumba ya kuishi.

"Pia kwa sasa nina uhakika wa matibabu. Kiukweli serikali iangalie namna ya kuwezesha zaidi mfuko huu TASAF," anasema Kashinde.

Maoni mengine ni ya mnufaika Khadija Kabututu, mkazi wa Kaza Roho mjini Tabora, anayeeleza kuwa aliorodheshwa kwenye mpango huo mwaka 2015, akipokea shilingi 42,000 kwa mwaka, ambazo baadaye ziliongezeka kufika shilingi 86,000.

Anasema pesa hizo aliziwekeza shambani, jambo lililomwezesha kuanzisha biashara ya kuuza matofali nayo kama alivyo mtangulizi wake, ameweza kujenga nyumba yake mwenyewe, pia akisomesha watoto.

AFYA

# Daktari ataja magumu ya utoaji mimba holela, mwanasheria ana adhabu yake

**Na Joyce Lameck**

HADI sasa katika jamii, kuna vilio vya mabinti kushiriki utoaji mimba, tena wakitumia njia zisizo sahihi kiafya na kisheria. Ni dhana ngumu inayowafanya mabinti kutafuta njia mbadala wa kutoa mimba zisizotarajiwa.

Mtaalamu bingwa wa tiba ya kinamama, Dk. Elias Kweyamba, anarejea matokeo ya utafiti mojawapo mwaka 2016, yalionyesha kila mwaka kuna kundi kubwa la wanawake wanaotumia njia potofu kutoa mimba zisizotarajiwa. Hiyo ni kutokana na sheria kukataza nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Elias Kweyamba, vifo vitokanavyo na uzazi usio salama, zinachangia hadi matukio ya vifo, kwa sababu ya kukosekana uelewa kuhusu uzazi salama.

Watafiti wanaainisha kila mwaka kuna kundi kubwa la wanawake nchini wanaopata mimba zisizotarajiwa na daktari huyo anataja takwimu, wengi ni mabinti wenye umri kati ya miaka 15 na 19.

Hapo ana ufafanuzi kwamba wengi ni kutokana na umri mdogo wanashindwa kuamua kwa busara, azma ya kubaki kwenye afya salama na inaelezwa hadi sasa, idadi kubwa ya mabinti hao ni wanafunzi wa ngazi tofauti kielimu.

Inaelezwa kuwa, rika hiyo inaangukia njia potofu za utoaji mimba, hata wanakumbwa na madhara kiafya, hasa katika mfumo wa uzazi wanatokwa na damu nyingi, pia kukiwapo ushuhuda wa matukio ya vifo kwa wahusika, wengine wanakwama kutekeleza malengo yao kimaisha.

Kweyamba anataja njia hizo zinazoripotiwa kutumika kutoa mimba, zinajumuisha miti ya mihogo, dawa ya kung'arisha mashati (blue), spoku za baiskeli, majani ya chai, pia majivu zinatajwa na madaktari, ukiwa ni uzoefu wao kutoka kwa wajawazito wengi wenye matatizo wanapowafikia.

Mbinu nyingine inayoripotiwa katika utoaji mimba huo wa kujitegemea, mtaalamu huyo anagusa matumizi ya dawa inayofanana na vichocheo vya mwili, yaani 'misoprostoli'. Vilevile anasema kuna uingizaji vifaa visivyo vya kiupasuaji kama sindano za tiba.

Kihistoria idadi ya mimea inayotumiwa kutoa mimba, ndio imetumika pia katika utabibu, japo si njia sahihi zinazomfanya mama abaki salama kiafya, moja ya vigezo vikuu ni vipimo vya matumizi ya dawa hizo kutokuwa sahihi.

Dk. Kweyamba anaainisha eneo lingine la madhara ya mbadala huo, ni uwezekano wa kusababisha madhara kama vile akili, ukitokana na msongo wa mawazo kwa mhusika, pia viungo vya mwili kukosa uwezo wa kufanya kazi, kama inavyotakiwa.



Hali ya mimba kwa mabinti, na wale ambao wamwefikia uzazi, katika picha tofauti. **PICHA ZOTE: MAKTABA**



Vilevile, anasema asilimia 25 ya wanawake walioko kwenye ndoa, wanakutwa na tatizo la ugumba, chanzo ikiwa ni utoaji mimba kabla, wakiwa wametumia njia zisizo salama kiafya.

Anarejea rekodi iliyoko ni kwamba, kinamama wengi wanapoteza maisha kwa kutotumia njia zisio sahihi, kwa sababu wanashindwa kupata huduma nzuri, pale wanapokuwa wanatoa mimba.

Hisia zao zinatajwa ni kwamba wanasita kufika hospitalini, wakihofu namna ya kujielezea, kabla ya kupatiwa huduma. Hilo nalo, linaingia katika hesabu ya kuwapo kundi la wanaopoteza maisha kwa kukosa huduma na wanaofika hospitalini, wakiwa wamechelewa kupatiwa huduma.

### WAATHIRIKA WANENA

Binti mmoja wa umri miaka 24 (jina lake limehifadhiwa) kwa sasa mkazi wa Mbezi Luis, Dar es Salaam, anaelezea namna alivyopata shida baada ya kutumia dawa za kutoa mimba, ikamfanya ashindwe kufikia malengo aliyojiwekea shuleni.

"Nilinunua dawa kwa dada ambaye hakuwa hata na duka la dawa, bali alikuwa ana duka la nguo pamoja na urembo wa wanawake. Lakini cha kushangaza, dawa hizo alikuwa nazo na ilionekana kuwa huwa anawauzia wanawake wengi.

"Baada ya kupatiwa dawa zile, bila ya kujua mimba yangu ilikuwa na miezi mingapi kwa kipindi hicho, matokeo yake nilitokwa na damu nyingi sana, maumivu ya tumbo makali na nilitokwa na harufu mbaya ... takribani ya miezi mitatu," anasimulia mhusika wa tukio hilo.

### MAONO KISERA

Shirika la Afya Duniani (WHO), lilitoa mwongozo mpya kuhusu huduma ya utoaji mimba, lengo ni kulinda afya ya wanawake na wasichana, kuzuia wastani wa mikasa milioni 25 duniani vya utoaji mimba usio salama kila mwaka.

Kurejea utafiti wa kisayansi wa WHO, mwongozo husika ukaibua zaidi ya mapendekezo 50 yanayohusu huduma za kitabibu, utoaji huduma za afya na uingiliaji kati kisheria na kisera, kusaidia matukio ya utoaji mimba yaangukie katika usalama.

Hata hivyo, kuna mtazamo kwamba kutokuwapo elimu na uhamasishaji wa kutosha wa afya ya uzazi kwa makundi mbalimbali na hasa vijana na wanaume, kumesababisha kuenea mimba zisizotarajiwa na kuongezeka magonjwa ya ngono, hasa vijijini.

Pia, kunatajwa mila potofu zimechangia kuzorotesha afya ya uzazi katika baadhi ya maeneo.

### SHERIA ILIVYO

Mwanasheria wa kujitegemea, Peter Majanjara, anaeleza namna utoaji mimba kwa wanawake wengi wanaotumia njia zisizo sahihi na sheria ya nchi haingalii mazingira halisi.

"Sheria haijaweka mazingira, kwa maana ya kwamba mtu amebakwa, amepata mimba kwa kujamiiana, basi anaweza kutoa mimba, sheria ya nchi hapo ipo kimya," anaeleza mwanasheria Majanjara.

Tamko la Sera ya Afya ya Mwaka 2007; serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itahakikisha "utoaji wa huduma bora za uzazi katika vituo vya kutoa huduma za afya zinazowavutia wanawake, wanaume na vijana."

Aidha, kisheria, utoaji mimba ni kosa la jinai na ina adhabu kali, hata inatajwa kuchangia baadhi ya wanawake kutumia njia za mafichoni.

Kimsingi, ni adhabu inayoweza kumfunga mtu, kulingana na uzito wa kosa husika, kisheria ikiwaangukia mhusika mkuu na anayeshiriki kutoa mimba kinyume na sheria.

Mwanasheria Majanjara, anasema kwa sasa kuna jitihada zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa nafasi zao, kushinikiza kupungua matukio ya utoaji mimba kwa njia zisizo sahihi.

Anasema, ili kutumia njia sahihi za utoaji mimba, kunatakiwa kuwapo mtu mwenye uelewa kitaalamu, pia mamlaka sahihi inayohusika kitabibu katika namna ya kumsaidia mwanamke mjamzito.

> **Sheria haijaweka mazingira, kwa maana ya kwamba mtu amebakwa, amepata mimba kwa kujamiiana, basi anaweza kutoa mimba, sheria ya nchi hapo ipo kimya.**

AFYA

# Ijue PID; ugonjwa unaomtesa mama, lakini wanaouelewa vilivyo wachache

**Na Mary Mbikiwa**

INAPOTAJWA 'Pelvic Inflammatory Disease' au kifupi PID, taafsiri yake katika lugha rahisi ni ugonjwa wa maambukizi ya vimelea kwenye viungo vya mfumo wa uzazi wa mwanamke.

Hapo, viungo vinavyoathiriwa zaidi ni shingo ya kizazi, mirija ya uzazi, tumbo la uzazi (uterasi) na mifuko ya mayai aliyo nayo mwanamama.

Ugonjwa wa PID unatajwa kuwapata wanawake wenye umri wowote, lakini kwa kiwango kikubwa wenye umri kati ya miaka 20 mpaka 40 ndio wanaoathiriwa zaidi.

Sababu kuu ya ugonjwa huo kuendelea kuwasumbua wanawake wengi, ni pamoja na kufanya ngono isiyo salama au kujamiiana bila ya kutumia kinga, maarufu kitaalamu 'ngono zembe'.

Ugonjwa huo kwa kawaida husababishwa na maambukizi ya vimelea na wapo wa aina nyingi wanaosababisha shida hiyo ya PID na mara nyingi inakuwa na uwiano wa kawaida wa vimelea kwenye uke unakuwa umevurugika, hivyo kuruhusu vimelea hatari kuzaliana.

Wanawake ambao wamewahi kuugua kisonono, klamidia, au magonjwa ya zinaa, wanatajwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kupata ugonjwa huo.

Mambo mengine ambayo yanaweza kuongeza hatari ya PID ni pamoja na kufanya ngono kabla ya umri wa miaka 18, kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja, pia kufanya mapenzi bila kutumia kinga.

Hata vivyo, kuna viashiria vya ugonjwa huo, kwa baadhi ya wanawake wenye ugonjwa wa PID wanaweza wasionyeshe dalili zozote, huku wengine ambao wanasumbuliwa na ugonjwa huo, wanaweza kuonyesha dalili zifuatazo:

Kuna maumivu kwenye tumbo chini ya kitovu; kutokwa na uchafu mweupe mzito sehemu ya siri kwa mwanamke, ikiwa na rangi ya maziwa mtindi; wengine hutokwa na uchafu wa rangi ya njano; pia, wapo wanaotokwa na uchafu wenye harufu ya shombo la samaki.

Hata hivyo, baadhi yao huhisi maumivu wakati wa kujamiiana, maumivu ya nyonga, kutokwa na damu ya 'mabonge mabonge' wakati wa hedhi, kutokwa na majimaji mengi ukeni yenye harufu mbaya; kuvurugika kwa siku za hedhi, maumivu wakati wa kukojoa na wakati wa kujisaidia haja kubwa.



Mgonjwa anayesumbuliwa na PID, akilalamika. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Ugonjwa huo kitaalamu unaelezwa unaweza kusababisha shida nyinginezo; maradhi ya 'Kansa ya Shingo ya Kizazi' au uvimbe kwenye mayai ya mwanamke.**



Daktari akimhudumia anayeugua maradhi PID

Mengine yanatajwa kitaalamau, ni kuwa na ukavu kwenye sehemu za siri, kupata maumivu ya mgongo, kutokwa na damu wakati wa tendo la ndoa au baada ya kujamiiana.

Pia, inatajwa kuna wakati mwanamke mwenye dalili hizo huwa anahisi hali ya kichefuchefu na kutapika kama mjamzito, homa kali, uchovu, kizunguzungu na kukosa hamu ya kula.

### UTAMBUZI NA TIBA

Jinsi ya kutambua mgonjwa wa PID, ishara kuu ni utambuzi wa ugonjwa huo hutokana na dalili za mgonjwa, daktari anafanya uchunguzi wa sehemu za siri za mgonjwa.

Namna ya uchunguzi na anachotambua tabibu, ndicho kinachoamua kuchukuliwa sampuli za maji au usaha kutoka sehemu za siri, ili kutambua aina ya vimelea anayesababisha maambukizi ya ugonjwa.

Madhara ya ugonjwa wa PID kwa mwanamke, yanaweza kusababisha maambukizi katika viungo vya uzazi na kusababisha ugumba au kutokuwa na uwezo wa kupata ujauzito.

Inaelezwa, namna mgonjwa anavyozidi kukaa na hali hiyo au kupata maambukizi kwenye njia ya uzazi, ndiyo hatari ya ugumba inazidi kuongezeka na uwezekano wa kutopata mtoto baada ya hapo.

Hali ya kutunga mimba nje ya kizazi nayo inachangiwa na ugojwa huo. Mimba huweza kutunga nje ya kizazi, endapo maambukizi hayo yamesababisha makovu ndani ya mirija ya uzazi.

Makovu hayo husababisha yai lililopevushwa kushindwa kusafiri ndani ya mirija ya uzazi kuelekea kwenye mji wa uzazi.

Mimba nje ya uzazi, husababisha utokaji wa damu usio wa kawaida ambao hatari yake unaweza kukatisha uhai wa mwanamke.

Ugonjwa huo kitaalamu unaelezwa unaweza kusababisha shida nyinginezo; maradhi ya 'Kansa ya Shingo ya Kizazi' au uvimbe kwenye mayai ya mwanamke.

Mvurugiko wa homoni nao huweza kusababisha mwanamke kupata hedhi ya muda mrefu au kukosa kuona hedhi kabisa.

Hapo napo inajitokeza suala la maumivu ya tumbo chini ya kitovu. Mwanamke mwenye maambukizi ya ugonjwa huo, huwa anasumbuliwa kila mara na maumivu chini ya tumbo.

### HATUA ZA KINGA

Hata hivyo, inatajwa kuna njia za awali za kujikinga na ugonjwa huo, pale mwanamke anahimizwa kuwa na mpenzi au mwenza mmoja, na akijua historia yake ya mahusiano yaliyopita, kutumia kinga wakati wa kushiriki tendo la ndoa.

Mwanamke anashauriwa kumshauri mwenza wake kupima afya yake dhidi ya magonjwa ya zinaa, pia virusi vya Ukimwi, kabla ya kuanzisha uhusiano naye.

Hata hivyo, daktari wa kinamama wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, Benjamini Kimaro, anashauri kitabibu mwanamke mwenye maradhi ya PID, hatua bora ni vema hatua yake ya awali ni kuwahi kwenye kituo cha afya ili apate tiba na kuepuka madhara kama ya ugumba.

Dk. Kimaro anasema, jamii nayo kwa ujumla inapaswa kutambue kuopata elimu ya chanzo kikuu chja maradhi PID na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa, katika jitihada za kuepuka ugonjwa huo.

Hapo ni namna inayoacha ujumbe wenye kipaumbele kwa wanawake wa Kitanzania, washirikiane kupeana elimu na maelekezo kwa watoto wa kike, hali itakayosaidia kuepusha ugonjwa huo.

Mtazamo na ujumbe mahsusi ni kwamba; "unapomuelimisha mtoto wa kike, unakuwa umekita kwenye mizizi au kiini cha ugonjwa huo", kwani watakuwa chachu au msaada kwa wengine.

***Makala hii ni kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya afya.***



# Machinga 45,283 kupatiwa vitambulisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema wafanyabiashara wadogo maarufu machinga 45,283 wamesajiliwa kwenye mfumo ili kupatiwa vitambulisho vya kidijitali na kufikia fursa za kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri Gwajima aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, utambuzi na usajili wa wafanyabiashara hao maarufu kama machinga, ulianza Machi mwaka huu na leo vitambulisho hivyo vitazinduliwa katika Mkoa wa Arusha ili vianze kusambazwa kwa walengwa.

"Zoezi la utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogo ni muhimu kwa kuwa litawezesha serikali kupata takwimu sahihi ya kundi hili ambalo linajumuisha machinga, mama na babalishe, wasusi, waendesha pikipiki za miguu miwili na miguu mitatu pamoja na makundi mengine ya wafanyabiashara ndogo," alisema.

Alisema kati ya wafanyabiashara hao wanaume 15,909 na wanawake 29,374, wametengenezewa kitambulisho kila mmoja na kudumu kwa miaka mitatu kwa Sh.20,000.

"Sh. 20,000 inayolipwa na mfanyabiashara ndogo wakati anasajiliwa ili kuchapishiwa kitambulisho hicho sio mbadala wa ada na tozo zinazotozwa na mamlaka za halmashauri hapa nchini katika maeneo biashara ndogo zinapofanyika," alisema Waziri huyo.

Alisema sekta ya wafanyabiashara hao inahusika pia kwenye kuchangia ukuaji wa uchumi nchini na kusaidia kutatua changamoto ya ajira kwa vijana

**Alisema sekta ya wafanyabiashara hao inahusika pia kwenye kuchangia ukuaji wa uchumi nchini na kusaidia kutatua changamoto ya ajira...**

Alitaja faida za vitambulisho hivyo kuwa ni kutumika kama dhamana kukopa mikopo yenye masharti nafuu itakayotolewa na serikali kupitia benki.

"Faida nyingine ni kuunganishwa na mifumo mbalimbali mfano mifumo ya kibenki, mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kadri ya makubaliano ya serikali na wafanyabiashara ndogo ili waweze kunufaika na fursa za mikopo yenye masharti nafuu kupitia taasisi za fedha na pia aweze kuweka akiba ya uzeeni kwa kadri watakavyokuwa wanachangia kwenye mifuko hiyo," alisema.

Alisema mamlaka kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi, wakurugenzi wa halmashauri nchini na taasisi za fedha wapo tayari kushirikiana na serikali kuhudumia kundi hilo.

"Zoezi la utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogo kwenye mfumo linasimamiwa na maofisa wa serikali kwa kila halmashauri kupitia dawati la kuratibu shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara hao kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa nchini," alisema Gwajima.

Aliwaomba wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kushiriki kikamilifu kusimamia zoezi hilo kitaifa ili lifanikiwe.




Wakili wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Isabell Nchimbi akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Mwanamke wa Kijijini, yaliyofanyika kitaifa, Nkulabi, Kata ya Mpunguzi, Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TRA yazindua ofisi ya walipakodi binafsi

**Na Mwadishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imezindua ofisi maalamu itakayohudumia walipakodi binafsi wenye hadhi ya juu huku ikiwahakikishia huduma bora.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ofisi hiyo iliyoko jijini Dar es Salaam, Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alisema hatua hiyo ni kuendelea kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiyari.

"Ninayo furaha kuungana na nyie kuja kuizindua ofisi ya walipakodi binafsi wenye hadhi ya juu iliyoanza kazi Oktoba Mosi, mwaka huu," alisema Mwenda.

Alisema ofisi hiyo itakuwa ikihudumia makundi manne ambayo ni wamiliki wa kampuni kubwa zinazozalisha zaidi ya Sh. bilioni 20 kwa mwaka, wamiliki wa hisa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.5 kwa mwaka, wenye ubia katika kampuni zinazozalisha zaidi ya Sh. bilioni 20, viongozi wa mihimili mitatu ya juu na wa taasisi watakaoteuliwa.

Alisema ofisi hiyo inawalenga walipakodi hao kwa sababu wanataka kuwapatia huduma bora kwa kutambua mchango wao na unyeti wa shughuli zao.

Alisema sababu kubwa ya kuanzishwa ofisi hiyo ni mchango unaotolewa na makundi hayo kwani kushindwa kuyapa huduma stahiki kutasababisha serikali kupoteza mapato na uchumi wa nchi kushuka.

"Kwa kuanza tumeanza na walipakodi 158, lakini walipakodi wamiliki binafsi wapo 111 wote wameshaitwa na viongozi wa mihimili mitatu ya juu ya serikali na wa taasisi 47 watakuja baadaye," alisema Mwenda.

Alibainisha mamlaka imeanza na idadi hiyo kwa kuwa ndio waliokidhi vigezo vya kuhudumiwa katika ofisi hiyo.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mcha Hassan Mcha, alisema ofisi hiyo ni miongoni mwa fursa ya kusogeza huduma karibu na walipakodi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

## Dendego awasihi wanafunzi kuzingatia masomo

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amezindua kampeni ya 'Tuwaambie kabla Hawajaharibikiwa' na kuwataka wanafunzi wa sekondari na vyuo mkoani hapa kuzingatia masomo ili waisaidie nchi kuleta maendeleo.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi huo uliofanyika Chuo cha Uhasibu (TIA), Tawi la Singida, Dengego, alisema wanapaswa kutumia muda wao kutafuta maarifa na si matumizi ya dawa za kulevya, mapenzi ya jinsia moja na vitendo vingine kinyume na maadili ya Mtanzania.

"Unapokuwa chuoni, hakikisha unatamani kuiona kesho iliyo nzuri, timiza ndoto yako ya kuwa na maisha bora, usidanganywa na mwenzako, simama na msimamo wako thabiti...leo hii mzazi amekuleta hapa huku akitarajia matokeo makubwa kwa maisha yako ya baadaye," alisema.

Aliwataka wanafunzi hao kushirikiana na Jeshi la Polisi kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsi kwa kutoa taarifa ili kuwabaini wahusika na kuwakamata na kuchukuliwa hatua.

Awali, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Mayunga Raphael Mayunga, alisema kampeni hiyo, itasaidia kuliweka kundi hilo mahali salama dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, ulevi, ukahaba na ushoga.

Aliwasihi wanafunzi kuwa na marafiki wenye tabia nzuri badala ya ambao wanaweza kuwaingiza kwenye msongo wa mawazo.

## Wanawake vijiji wasota kumilika ardhi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAWAKE vijijini bado wanakabiliwa na tatizo la mila, desturi potofu na mfumo dume na kukosa haki za msingi za kumiliki mali na ardhi.

Hayo yalibainishwa jana na baadhi ya wanawake kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke anayeishi kijijini iliyofanyika Kijiji cha Nkulabi jijini hapa yaliyoandaliwa na Chama cha Mawakili Wanawake nchini (TAWLA).

Wanawake hao, walisema wanaendelea kunyimwa haki ya kumiliki ardhi kutokana na mila na desturi potofu.

Rehema Simoni, aliwaomba wanasheria kushirikiana na serikali na taasisi za dini kutoa elimu itakayosaidia jamii kuondokana na mfumo dume.

Wakili wa TAWLA, Isabela Nchimbi, alisema kuwa chama hicho kimekuwa kikipokea malalamiko kuhusu haki za msingi kwa ajili ya wanawake waishio vijijini. Alisema kuwa miongoni mwa malalamiko ni pamoja na kunyima haki zao za kumiliki adhi hii ni pamoja na mtoto wa kike kwa madai kuwa mwenye haki ni mwanaume na mtoto wa kiume, hivyo bado kunahitajika elimu zaidi.

Khadija Mrisho, mtaalamu wa masuala ya ardhi kutoka Shirika la Landesa, alisema changamoto kubwa wanayoipata wanawake vijijini ni wanaume kuamini kuwa uhalali wa kumiliki ardhi ni makosa.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: INSPECTION ENGINEER**

**Reports to:** N+1: Inspection Lead, N+ 2: Head of Maintenance and Inspection

**Job Type:** Full Time- 5d/w - with regular duty week and frequent EACOP site visit

**Location:** MST – Tanga (prior site readiness location will be Dar es Salaam and construction sites)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

The Inspection Engineer will support the EACOP Inspection Leader. He will cooperate with a team of 4 inspections specialists or engineers. He will be the interface for inspections activities between pipeline engineer, corrosion engineer, site method, contractors, and authorities. **EACOP main equipment under inspection responsibility are:**

- Pipeline
- Vessel: Pig Receivers, Pig Launcher, drain drums, air vessels, Nitrogen cylinder, pressures vessels
- Fire heaters
- Structures: Exhaust stack, LOF, Communication Towers
- Storage tanks
- Lifting equipment and structures.
- Piping
- EPRS

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Establishes inspections services contract required for EACOP inspection plan.
- Analyzes and optimizes inspection activities efficiency.
- Reviews management of change request.
- Follow up and update Risk base inspection tools for piping and vessel.
- Ensures lifting register, flexible register, temporary repair database is up to date.
- Ensures welding qualification, material and procedure required for Pipeline emergency repair are available and up to date.
- Be the focal point for inspection and corrosion exchange.
- Reviews Inspection program, and partial Field shutdown
- Reviews the Inspection Reports, including analysis of inspection findings, fit for service assessment, recommendation for remedial actions.
- Participates in technical audits of contracted companies regarding Non-Destructive Testing, Welding, Piping/Pressure Vessel fabrication, Coating.
- Reviews the recommendation for corrective actions (material selection, design of equipment, coating, cathodic protection, operating conditions, corrosion inhibition…)
- Ensures that repair / modifications / procurement of equipment complies with the relevant regulation, company rules, technical codes, and norms.
- Prepares inspection scope and campaign, with a follow-up of the performance of the team and objectives including monitoring of KPI's (progress, budget, etc…)
- Analyzes degradation modes or reports to be reviewed with Inspection Leader.
- Acts as Inspection lead deputy during inspection lead leave.
- Audits regularly required contractor and site.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

- **Academic Qualifications:**
- Bachelor level or similar.
- Mechanics or Materials Engineer (or equivalent) with emphasis on mechanics, materials, metallurgy, and corrosion.
- Knowledge of Oil & Gas process equipment, technology, and piping
- Good knowledge of international Codes, Standards and Regulation related to the inspection discipline (ASME, API, NACE…)
- Good knowledge of materials, metallurgy, welding, corrosion, failure modes, Non-Destructive Testing, and inspection techniques.
- Knowledge of RBI methodology (Risk Based Inspection.)
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System.)
- Good knowledge in Fitness for Service assessment methods (API RP 579, ASME, DNV…)
- Proficiency in oral and written English.
- ERB Registration as a Professional Engineer.
- **Experience Required:**
- Minimum 6 years' experience as supervisor or leader in inspection related activities in the Oil & Gas industry or Refinery or Petrochemical Site.
- Experience in Full Field shut down inspection scope preparation and follow up.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: INSPECTION LEAD**

**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and Inspection, N+ 2: Field Operations Manager

**Job Type:** Full Time

**Location:** MST - Tanga

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

- The Inspection Leader will be the head of EACOP inspection entity. He will manage a team of 5 inspections specialists: pipeline, corrosion, site, method, and contracts required to follow inspection plan.
- Inspection philosophy will be established by the Inspection Leader.
- The Inspection Leader will ensure proper coordination, organization, and process to maintain asset mechanical integrity.
- He/she will validate inspection scope and campaign, with a follow-up of the performance of the team and objectives including monitoring of KPI's (progress, budget, etc…)
- An extensive experience Coaching of new Inspection Engineers regarding damage mechanisms and inspection techniques and will support to create the EACOP inspection referential.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Defines and reviews maintenance inspection philosophy.
- Establishes contact, processes, audit plan according to Standard, local requirement, and authorities.
- Participates in recruitment process and selection of inspection team.
- Establishes inspections services contract required for EACOP inspection plan.
- Coordinates Tanzania and Uganda inspections entities.
- Analyzes and optimizes inspection activities efficiency.
- Reviews management of change request.
- Selects and review Risk base inspection tools required for EACOP asset.
- Ensures lifting register, flexible register, temporary repair database is up to date.
- Ensures welding qualification, material and procedure required for Pipeline emergency repair are available and up to date.
- Be the focal point for inspection and corrosion exchange.
- Reviews Inspection program, Intelligent pigging operation and partial field shutdown.
- Participates in the Maintenance Inspection Budget preparation.
- Reviews the Inspection Reports, including analysis of inspection findings, fit for service assessment, recommendation for remedial actions.
- Participates in technical audits of contracted companies regarding Non-Destructive Testing, Welding, Piping/Pressure Vessel fabrication, Coating.
- Reviews the recommendations for corrective actions (material selection, design of equipment, coating, cathodic protection, operating conditions, corrosion inhibition…)
- Ensures that repair / modifications / procurement of equipment complies with the relevant regulations, company rules, technical codes, and norms.
- Manages team and resources.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

- **Academic Qualifications:**
- Bachelor level or similar Mechanics or Materials Engineer (or equivalent) with emphasis on mechanics, materials, metallurgy, and corrosion.
- Knowledge of Oil & Gas process equipment, technology, and pipeline.
- Good knowledge of international Codes, Standards and Regulation related to the inspection discipline (ASME, API, NACE…)
- Good knowledge of materials, metallurgy, welding, corrosion, failure modes, Non-Destructive Testing, and inspection techniques.
- Knowledge of RBI methodology (Risk Based Inspection.)
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System.)
- Good knowledge in Fitness for Service assessment methods (API RP 579, ASME, DNV…)
- Proficiency in oral and written English.
- **Experience Required:**
- Minimum 10 years' experience as supervisor or leader in inspection related activities in the Oil & Gas industry or Refinery or Petrochemical Site.
- Experience in Full Field shut down inspection scope preparation and follow up.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

## HABARI ZANZIBAR

# Waziri atangaza utalii angani, aruka kwa parachuti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, ameongoza wananchi kuruka angani kwa kutumia parachuti ikiwa ni sehemu ya kutangaza vivutio vya utalii visiwani hapo.

Zoezi hilo lilianza katika Uwanja wa Ndege Kigunda Mkoa wa Kaskazini Unguja hadi fukwe za Bahari ya Hindi Kwendwa.

Akizungumza baada ya kuruka umbali wa futi 10 kutoka usawa wa Bahari ya Hindi kuelekea angani Soraga, alisema unaambatana na utambulisho wa Mkutano wa Maonesho ya Utalii na Uwekezaji unaotarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwaka huu visiwani hapa.

"Dhumuni la tukio hili la leo lina mambo mawili, kwanza katika wizara tuna usemi wetu wa kutangaza utalii kwa vitendo na kutangaza utalii kwa vitendo ni kuonekana katika vivutio vya utalii na kufanya matukio ambayo yataleta watalii," alisema Sora.

Alisema kivutio cha parachuti ni sehemu ya utalii kwa kutangaza fursa zilizoko Zanzibar, ikizingatiwa ni nchi nzuri kutokana na madhari na mazingira yake.

Akizungumzia mkutano huo, alisema unatarajiwa kuhudhuriwa na wadau zaidi ya 200.

Mdhibiti Ubora wa Kampuni ya Afrika Skydive, alisema kufanyika kwa zoezi hilo kutokana na viwango vya kimataifa ambalo linadhaminiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA), viwango vya kitaifa na kimataifa.

# Wataalamu ganzi, usingizi kuula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema Wizara ya Afya itahakikisha wataalamu wa ganzi na usingizi wanawekewa mazingira bora ya kufanya upasuaji salama kwa wagonjwa katika hospitali za visiwani hapa.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wataalamu wa Ganzi na Usingizi Duniani yaliyofanyika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil Kikwajuni.

Abdulla, alisema serikali itahakikisha inawawekea mazingira bora wataalamu hao, kuwapatia maslahi, stahiki zao na fursa za kwenda kusoma ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea ujuzi.

Hemed, alisema kuboreshwa na kuimarishwa kwa sekta ya afya nchini hususan katika kada hiyo kutarejesha hadhi na heshima ya kundi hilo na kutawavutia vijana wengi zaidi kutoa huduma hospitalini.

> **Waziri wa Wizara ya Afya, Nassor Ahmed Mazuri, alisema awali wajawazito wengi walikuwa wanafariki na watoto chini ya miaka mitano walikuwa wakiathiriwa...**

Makamu huyo wa pili, aliutaka uongozi wa wizara hiyo na wataalamu hao kuzifanyia kazi changamoto zinazokabili kada hiyo ili kuboresha utendaji kazi wao.

Hata hivyo, alisema wakati umefika kwa wizara hiyo kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuanzisha kada hiyo kwa kuwa imekuwa na uhitaji mkubwa wa wataalamu visiwani hapa. Vilevile aliwataka wataalamu wa afya kuendelea kutoa huduma kwa kufuata maadili, kuwa na upendo, huruma na moyo wa kujitolea kwa wagonjwa.

Abdullah, alitoa wito kwa wanafunzi wanaomaliza ngazi ya diploma ya uuguzi kuwa tayari kujiunga na kada hiyo ili kukabiliana na uhaba wa wataalamu.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazurui, alisema wamejipanga kuimarisha na kuboresha taaluma ya ganzi na usingizi kwa kuwasomesha na kuwaendeleza watendaji na kununua vifaa vya kisasa kusaidia kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mazrui, alisema kada hiyo imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa, wasaidizi na vifaa tiba vya kisasa.

Alisema Zanzibar ina madakatari bingwa wa ganzi na usingizi wanne ambao hawatoshelezi kutoa huduma kwa wagonjwa kufanyiwa upasuaji.

Akisoma risala katika maadhimisho hayo mtaalamu wa huduma hiyo, Dk. Sabrina Abdalla Ali, alisema kada hiyo imekosa kutambulika rasmi kama nyingine kutokana na kukosa usimamizi na mfumo rasmi wa utendaji wa kazi.

Alitaka wizara hiyo kutoa kipaumbele katika kuwaendeleza kimasomo watendaji wa kada hiyo na kuwashawishi wanafunzi kusomea kwa maslahi ya taifa.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kinondoni, Furaha Michael (kulia), akitoa elimu ya masuala mbalimbali ya mikopo kwa vijana wanufaika wa Mradi wa 'Going Beyond' wa DOT na Taasisi ya Mastercard Foundation, unaotekelezwa na Asasi ya Her Initiative, wakati wa mkutano uliowakutanisha vijana hao na watoa huduma za maendeleo ya kibiashara, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Uzalishaji hiliki washuka wilayani Muheza

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** MUHEZA

MABADILIKO ya tabianchi yanadaiwa kusababisha uzalishaji wa hiliki kushuka wilayani hapa Mkoa wa Tanga na kusababisha wakulima zao hilo kukosa kipato.

Hayo yalisemwa na Kaimu Ofisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Nyenza Adam Michael, wakati akizungumza na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) walipokuwa wilayani hapo kwa ziara ya mafunzo na kuangalia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia mradi wa Shirika la Misaada la Umoja wa Mataifa Marekani (USAID) wa Tuhifadhi Maliasili.

Michael, alisema zao hilo linahitaji mvua na mbolea za kutosha kutoa mavuno mengi na kuongeza kipato kwa wakulima.

"Karibia miaka mitano sasa uzalishaji wa hiliki umeshuka sana kwa sababu ya ukosefu wa mvua na mbolea na zao hili linahitaji mbolea sana," alisema.

Alitaja hatua wanazozichukua kuwa ni kutoa elimu kwa wakulima ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kujihusisha na kilimo rafiki kwa mazingira.

Alisema wamewafundisha wakulima hao kutengeneza makinga maji ili kuhifadhi unyevu kwa muda mrefu na matumizi ya samadi.

Alisema wanawafundisha kupanda kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo na kuhudumia shamba kwa nafasi kwa kufanyiwa usafi ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema wilaya hiyo ilikuwa inazalisha wastani wa tani 200 za hiliki kwa mwaka na kwa sasa ni tani 2,600.

Alisema baada ya miaka mitatu wanatarajia uzalishaji wa zao hilo utaongezeka na kufikia tani 4,000 kwa mwaka.

Alisema soko la hiliki ni kubwa na kuna uhitaji mkubwa wa hiliki ambapo kilo moja ya hiliki ni shilingi 30,000.

Msimamizi wa Mradi wa Kilimo Hai wa GFP Organics Limited katika halmashauri hiyo, Magreth David, alisema kilimo hai ni mlinzi mkuu wa mazingira na kwamba kinasaidia kudhibiti uchomaji moto misitu na ukataji miti.

"Ukichoma msitu unaondoa uasili wa eneo, pia huwezi kupata majani mazuri ya kulisha mifugo ambayo kinyesi chake ni mbolea," alisema.

Alisema Tuhifadhi Maliasili, umesaidia kutoa elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uzalishaji wa mazao ya viungo.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wakulima Hai Kijiji cha Kwezitu, Emmanuel Mkufya, alisema mradi huo umewasaidia kufahamu namna ya kulima kilimo hai, kutunza mazingira na kujipatia kipato cha uhakika na uhakika wa kuuza mazao yao.

Muheza hasa katika Tarafa ya Amani, kwa wakazi wake na Kijiji cha Kwemhosi kimebeba simulizi ya kilimo hai, ikiwamo kilimo cha viungo cha hiliki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**JENIFER SALINJA KILIMA** anatangaza kupotea kwa Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0216/0743** iliyotolewa na **NGANZA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2024. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/224210/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TATU JAMES ROBERT** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S. 3794/0632** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Nyankumbu Girls Secondary School mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/GEI/GEI/9065/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN FRANCIS KIDASI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0154-0023,** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST. PETER'S SEMINARY SCHOOL mwaka 1996. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **MBE/MBE/74540/2022**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**TWAIB ABDULHAFFIDH TWAIB** anatanganza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE142731** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM mnamo tarehe 18/07/2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/224593/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SEMENI MUSSA NANDONDE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071-0119** kilichotolewa na **ST. MATHEW'S SECONDARY SCHOOL** mwaka 2006. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1599-0569** kilichotolewa na **BAOBAB SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009. Cheti cha chuo chenye Reg. No. **BAEC 11711** kilichotolewa na **SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA** mwaka 2012. Cheti cha Matokeo (TRANSCRIPT) Reg. No. **BAEC 11711** 2009-2012. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/223914/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAVID NELSON NGESI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S0500/0105** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **WANIKE SECONDARY** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/4806/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ATHUMANI OMARI SHEKIMOSHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 989 CAQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/10586/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANNETH ENOCK MWASULUKA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T466 DFY**
AINA YA FUSO MITSUBISHI YENYE CHASISI NAMBA **MEC2411BAFP012834**
KWAYEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/15998/2024.**

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili 110750**

Wamiliki wa kampuni ya AFRI ASIAN TRADING LIMITED, Namba ya Usajili 110750 iliyopo katika ofisi yenye plot No.14 ,Michungwani Street Muheza Road,Tanga,Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa Inatarajia kufanya kikao chake cha mwisho chakufunga kampuni cha Tarehe 2/9/2024 basi kupitia taarifa hii mwenye madai au malalamiko dhidi ya kampuni afike ofisini kuwasilisha taarifa za madai yake au malalamiko kabla ya kufungwa kwa kampuni.

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili 110750**

Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa kampuni ya AFRI ASIAN TRADING LIMITED Imemteua Mfilisi wa kampuni LINDA ELIUD LUGANO wa S.L.P 2228 Tanga-Tanzania atakuwa anahusika na shughuli zote za ufilisi wa kampuni kwakipindi cha taratibu za kufunga kampuni.

**Asante**
**Mkurugenzi wa Kampuni**

## AFRI ASIAN TRADING LIMITED

**Namba ya Usajili 110750**

Wamiliki wa kampuni ya AFRI ASIAN TRADING LIMITED, Namba ya Usajili 110750 Iliyopo katika ofisi yenye plot No.14 Michungwani Street Muheza Road, Tanga, Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa Inatarajia kufanya kikao chake cha Kwanza cha kufunga kampuni cha Tarehe 7/9/2024,basi kupitia taarifa hii mwenye madai au malalamiko dhidi ya kampuni afike ofisini kuwasilisha taarifa za madai au malalamiko kabla ya kufungwa kwa kampuni.

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Upinzani wapendekeza Ramaphosa ashtakiwe

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

KIONGOZI wa Chama cha Umkhonto we Sizwe amesema hatua ya mkurugenzi wa mashtaka ya umma jimboni Limpopo kutomshtaki Rais Cyril Ramaphosa, katika sakata tata la ufisadi na utakatishaji fedha ni aibu kwa taifa hilo la Afrika Kusini.

Kiongozi huyo wa chama hicho Dk. John Hlophe, alisisitiza jana kuwa Rais Ramaphosa ana kesi ya kujibu, ikiwa ni pamoja na tuhuma za kukwepa kulipa kodi.

Chama cha Wapigania Uhuru wa Kiuchumi (EFF), chini ya mwenyekiti wake Julius Malema, pia kilisema kina ushahidi wa kutosha kumfungulia mashtaka Rais Ramaphosa na kimepanga kuwasilisha hoja bungeni ili wabunge wapige kura ya kutokuwa na imani na Rais.

Hii ni katika mazingira ambako mjadala unaendelea kuzua hisia miongoni mwa wananchi, huku wengi wakihoji ni kwanini mkurugenzi wa mashtaka ya umma aliamua kumfutia kesi Rais.

Wakati huo huo, maswali yanaibuka kuhusu kitita cha dola milioni nne kilichopatikana kimefichwa chini ya makochi badala ya kupelekwa benki. Na kwamba sakata hilo linaweza kuwa na athari kubwa kwa utawala wa Rais Ramaphosa, ambaye anakabiliwa na kashfa kadhaa zinazohusiana na ufisadi. Malema alisema kuwa kesi ya wizi na utakatishaji fedha iliyofutwa na mwendesha mashtaka wa jimbo la Limpopo ni mwanzo tu.



"Siku ya Ramaphosa mahakamani inakuja pamoja na mamlaka huru ya mwendesha mashtaka. Bunge linaweza kupita na Ramaphosa akashtakiwa kwa sababu unaweza kupigiwa kura ya kutokuwa na imani hata ukiwa umetoka madarakani," alisema.

Mwaka 2020, mkuu wa zamani wa kitengo cha ujasusi alizungumzia malalamiko ya jinai dhidi ya Ramaphosa kuhusu madai ya wizi wa dola milioni nne katika shamba lake la Phala Phala. Na kwamba uchunguzi wa kitengo maalum cha polisi ulishindwa kumfungulia mashtaka yeyote, hatua iliyosababisha hasira miongoni mwa wanasiasa na umma.

Mwendesha mashtaka wa Limpopo, Mukhali Thenga, alisema kuwa ni muhimu Rais ashtakiwe kutokana na ukweli kwamba fedha hizo hazikuwekwa wazi kwa umma, huku akisema "Rais ana hatia ya kukwepa kulipa kodi".

Ilielezwa kuwa Rais wa awamu ya pili baada ya utawala wa ubaguzi wa rangi, Thabo Mbeki, aliondolewa madarakani baada ya chama chake kumtaka aachie ngazi, na mrithi wake, Jacob Zuma, naye alikumbana na kashfa za ufisadi.

Mchambuzi wa siasa Mudeba Fisto alitoa wito wa kufuatilia sakata hilo kwa ukaribu. "Ni muhimu kulifuatilia, kwani linaweza kuwa na athari kwa rais mwingine atakayefuata," alisema.

Hata hivyo, Mahakama ya Katiba tayari imekubali kusikiliza maombi yaliyowasilishwa na EFF na chama cha ATM, ambapo vyama hivyo vinaitaka mahakama ichunguze hatua za bunge kuhusu kesi ya kumtimua madarakani Rais Ramaphosa. **DW**

# Mahakama yagoma kuingilia kumwondoa Gachagua

**NAIROBI,** Kenya

MAHAKAMA ya Rufani nchini Kenya chini ya jopo la majaji watatu imekataa kuingilia kati mchakato wa kuondolewa madarakani Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua kupitia ombi lake la kuzuia mchakato huo ikisema kuwa utaendelea kama ulivyopangwa bila kuingiliwa.

Mahakama hiyo ilitoa msimamo huo jana baada ya kufanya kikao kilichochukua saa kadhaa, huku Majaji Erick Ogolla, Antony Mrima na Frida Mugambi wakisema hakuna suala lolote litakalomkuta Gachagua iwapo Bunge la Seneti litaendelea na hoja ya kumtimua katika wadhifa huo.

Pia majaji hao walisema uamuzi huo haumzuii Gachagua kukata rufani kuupinga katika korti nyingine kama hatoridhika nao na pia mahakama bado inaweza kuamua matokeo ya mchakato wa Bunge.

Wakijibu uamuzi huo, timu ya wanasheria wa Gachagua walitaka kurekebisha ombi hilo kulingana na kile ambacho kinaweza kushuhudiwa katika seneti.

Wanasheria hao wakiongozwa na Lempaa Soyinka walisema malalamiko yaliyorekebishwa hayatakuwa mapya na hakuna upande utakaobaguliwa bali walalamikiwa wanataka kuchelewesha kesi kwa kukataa marekebisho yao.

Upande wa wajibu maombi ukiongozwa na Benson Milimo, wakili wa Bunge la Kitaifa, alipinga ombi hilo akitoa mfano kuwa uamuzi huo hautakuwa wa haki ikiwa hawatafahamu undani wa marekebisho hayo.

Uamuzi huo wa Mahakama unaweka msingi wa kesi ya kumwondoa Gachagua kwenye nafasi yake kuendelea katika Bunge la Seneti ambalo limeshaanza kujadili kesi hiyo itakayosikilizwa kwa siku mbili kuanzia jana kabla ya kupiga kura ya kumwondosha au kumbakisha rasmi katika ofisi yake ya Naibu Rais.

Hata hivyo, mapema jana Gachagua aliwasili katika Bunge la Seneti kwa ajili ya kusikiliza mwendelezo wa majadiliano ya bunge hilo pamoja na kutoa utetezi wake lililoanza majira ya saa nne asubuhi huku likionekana kuzingirwa na ulinzi mkali wa polisi pamoja na usalama upande wa Naibu huyo wa Rais.

Matokeo ya mchakato huo yanatarajiwa kulifanya bunge la nchi hiyo kuketi tena kesho ili kujadilili na kupendekeza jina la mtu mwingine ambaye atachukua nafasi ya Gachagua kama seneti itaridhia kuondolewa kwake.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title:** INSTRUMENTATION & CONTROL SYSTEM ENGINEER

**Job Type:** Full Time

**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and Inspection
N+ 2: Field Operations Manager

**Location:** Tanga (prior site readiness location will be Dar es Salaam)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

- The job holder assists and supports, within the Field Operation team for all the maintenance and inspection activities related to the ICSS (Integrated Control and Safety Systems), Instrumentation and Telecom of the future EACOP facilities. He is responsible for all aspects related to ICSS and Instrumentation during the maintenance and inspection engineering phase and shall bring assistance on this subject as and when required. During operation, he will support the maintenance needs of instrument, ICSS, and telecom including associated services company and contracts.
- The job holder will pay particular attention to the identification and the right definition of the performance standard of the Safety Critical Element in his perimeter.
- The job holder is also accountable for demonstrating individually an exemplary behaviour regarding HSSE rules & requirements, and for ensuring their application within his scope of responsibility.

**Management:**

- Ensures Instrumentation, ICSS and Telecom support teams cover the obligations in term of maintenance strategy update, performance monitoring, contract, and stock strategy. Define priorities to focus on delivering values matching with Field Operations Objectives.
- Produces, reviews guidance documents, procedure, standard related to his perimeters.
- Follows ICSS major maintenance & Update.
- Ensures implementation of operation and maintenance strategy based on FO objectives. Ensure management system is up to date and in line with the Area performance objectives. Recover any REX from Area and analyse KPI to set-up maintenance strategy accordingly.
- Assess and audit CONTRACTOR procedure managing material repair in workshop are well implemented to secure reliable tracking system, follow-up, and progress.
- Ensures CONTRACTOR stock management by technology in line with criticality study, capability to repair and availability objective.
- Optimization: Review and challenge CONTRACTOR maintenance plan on instrumentation and ICSS and do proposal to reduce downtime and cost to optimize cost VS running hours.
- Secure life cycle management of equipment / packages; implement studies and action plan to secure maintainability of the plants (obsolescence.)
- Responsible for implementing and sustaining all cybersecurity solutions to guard industrial network against cyber-attacks.
- PI system Administrator for Field Operations. Manages PI sustenance and development to adequately cover rotating equipment, metering, and other requirements.
- OPEX: Cooperate with MAN head in terms of budget management for studies, ISS and modifications related to Service.
- Develops periodic reporting activities of the Discipline and follow them.

**Operations:**

- Recommends diagnosis & corrective actions related to major malfunctions and failures. Comments Contractor action plan and assess CONTRACTOR competencies and process to solve major malfunctions and failures. Support CONTRACTOR if required.
- Organizes and maintain instrument equipment database. Guarantee the quality of activity reporting, particularly though CMMS.
- Reliability: Responsible of COMPANY reporting regarding reliability improvement as a continuous practice to maximise plant availability; identify improvement opportunities in organization, facilities availability, and technical costs; represent progress in reliability meeting.
- Follow KPI's defined and attend / prepare for meetings, update dashboard upon requirement, provide action plan for reliability meeting…
- Develop positive and constructive relationships with contractors and suppliers. Identify opportunities to improve contractor/supplier performance, reduce costs and improve the quality of services/products supplied.
- Act as technical discipline focal point on specific project/work scopes and contracts, taking a lead role in the involvement/co-ordination of, and interface between, site/ teams/contractors ensuring effective communication and understanding between appropriate parties.

**Engineering Studies**

- Proposes solutions to optimize the operating cost.
- Consolidates ICSS & instrumentation part of Software Modification workflow issued by site dealing with ICSS and instrument discipline.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**In the context of teamwork and in the field of maintenance:**

- Shares and provides reliability analysis, optimization, and availability of equipment in line with the production objectives.
- Prepares and manages Contract technical need for the Maintenance contract team to implement on time in line with operation readiness planning.
- Defines maintenance policies and ensure international rules and standards followed according to his disciplines.
- Participates and updates REX and recommendation for future contract as EACOP strategy.
- Participates to contractor and subcontractor audits.
- Regular site visits.
- Adequate maintenance plans for related equipment and evidence of execution via CMMS
- Adequate material replenishment plans and effective liaison with C&P to always ensure required stock levels.
- Effective execution of assigned contracts.
- Availability, reliability, and obsolescence management of Instruments/PLC/ICSS/Metering systems.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Engineering Bac +5 level with specialization in ICSS or Instrumentation, or equivalent proven experience (Engineer)
- Industrial information security system training.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- Experience in instrument and ICSS maintenance and management (over 10 years), competence in cyber security, oil/Electric/production/terminal knowledge …
- Experience in industrial maintenance (over 8 years) and maintenance methods.
- Experience in team management.
- Very good knowledge of Instrumentation and Fundamentals of Legal Metrology in metering of petroleum products.
- Reliability, autonomy, analytical, organizational capacity, and leadership.
- Sense of method, flavor analysis, rigor, and organizational skills.
- Proficiency in English, both spoken and written.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

# MASHUJAA YAZIPIGIA HESABU SIMBA SC, KENGOLD LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha wanazibakisha pointi sita nyumbani, uongozi wa Mashujaa FC umesema unajipanga vyema kwa kuimarisha kikosi chao kuelekea mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata, imeelezwa.

**Mashujaa itawakaribisha KenGold kutoka jijini Mbeya Oktoba 21, mwaka huu halafu itawaalika Wekundu wa Msimbazi ifikapo Novemba Mosi, mechi zote zikitarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika.**

Akizungumza na gazeti hili, Meneja wa Mashujaa, Athumani Amiri, alisema kikosi chao kinaendelea na programu ya kujiimarisha na kwa sasa wachezaji wanafanya mazoezi ya 'gym' kwa ajili ya kuimarisha miili yao.

Amiri alisema wanataka kuona kila mchezaji anakuwa fiti kuelekea mechi hizo mbili ambazo zote zitakuwa ngumu kutokana na kila upande kujipanga vyema.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, malengo yetu ni kupata pointi tatu katika mchezo wetu dhidi ya KenGold ambao tutaucheza nyumbani kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, na baada ya hapo tutajipanga upya ili kuwakaribisha Simba," alisema Amiri.

Meneja huyo alisema morali ya kila mchezaji ipo juu na wameahidi wataonyesha viwango vya juu kwa sababu wanataka wanawapa burudani nzuri mashabiki pamoja na wanachama wao.

Aliongeza afya za wachezaji wake ziko vizuri isipokuwa wachezaji wawili ambao ni, Abdul Malik na Mohamed Mussa ambao wanasumbuliwa na maumivu ya nyama za paja.

"Wachezaji hao (Abdulmalik na Mussa), hawatakuwa katika sehemu ya mipango katika mechi inayokuja, ingawa wameshaanza kufanya mazoezi mepesi mepesi, naamini mchezo wetu dhidi ya Simba watakuwa tayari kuipambania timu," alisema meneja huyo.

Aliwaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kuishangilia timu ili waweze kupata ushindi.

"Malengo yetu ni kufanya vizuri katika mechi zote za nyumbani, tunawaomba mashabiki watusapoti, kwa pamoja tupambane kuhakikisha malengo yetu ya kumaliza msimu tukiwa katika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu yanatimia," aliongeza.

Alisema kila mechi kwao ni muhimu na wataingia uwanjani wakiwaheshimu KenGold ambayo pia wachezaji wake wameanza kucheza soka la kuelewana.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama kupisha Kalenda ya Kimataifa inatarajia kuendelea tena kuanzia Jumamosi kwa watani wa jadi, Simba na Yanga kukutana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## *Netiboli Muungano kufanyika Dar*

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Netiboli ya kuwania Kombe la Muungano yanatarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 28 hadi Desemba 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa nje wa Uhuru, Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Hilda Mwakatobe, aliliambia gazeti hili jana lengo la michuano hiyo ni kupata timu zitakazoiwakilisha nchi katika mashindano ya Afrika Mashariki yatakayofanyika baadaye mwakani nchini Uganda.

Mwakatobe alisema timu zinazotarajia kuchuana zinaendelea vyema na mazoezi na wanatarajia mwaka huu kutakuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

"Maandalizi kuelekea kwenye mashindano haya yanaendelea vizuri, kila timu inafanya mazoezi ya nguvu ili ipate nafasi ya kwenda Uganda, tutarajie kushuhudia upinzani mkubwa," alisema Mwakatobe.

Katibu huyo alisema jumla ya timu 12 tayari zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ambapo timu sita zinatoka Tanzania Bara na nyingine Zanzibar.

Alizitaja timu kutoka Tanzania Bara ni pamoja na JKT Mbweni, Uhamiaji, Jeshi Stars, Magereza, Polisi (Arusha) na Mapinduzi ya jijini Dodoma.

"Tunafurahi kuona wachezaji walionyesha viwango vya juu katika mashindano yaliyomalizika hivi karibuni mkoani Kilimanjaro na kushuhudia timu sita zikipanda daraja, mchezo huu unaimarika kila siku," Mwakatobe aliongeza.




Kiungo wa Yanga Princess, Danai Bhobho (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza hivi karibuni. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Mwembe Makumbi City yarejea kileleni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MWEMBE Makumbi City imefanikiwa kurejea tena kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Maafande wa Uhamiaji FC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja Nje wa Amaan (Annex B), juzi jioni.

Mechi hiyo ambayo ilikuwa ya ushindani na kuvutia, ilihudhuriwa na idadi kubwa ya mashabiki.

Kwa matokeo hayo, Mwembe Makumbi City inaongoza msimamo wa ligi hiyo baada ya kufikisha pointi 15 akifuatiwa na Mafunzo SC yenye pointi 13 sawa KMKM SC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mwembe Makumbi City, Rajab Mrisho, alisema siri ya timu yake kupata ushindi mfululizo imetokana na hamasa kubwa inaonyeshwa na wachezaji wao pamoja na mashabiki.

Mrisho alisema wachezaji wake wamekuwa wakielewa vyema mafunzo wanayowapa na hilo limechangia kupata ushindi katika mechi hizo tano walizocheza mfululizo.

"Wachezaji wetu wamekuwa wanaelewa somo la umuhimu wa kupata alama tatu, kwa kila mchezo ndio maana wanacheza kwa bidii ili wapate ushindi, lakini mashabiki wetu wamekuwa na sisi pamoja katika kila mechi tunayocheza, hili ni jambo la kuwashukuru na kuwapongeza," alisema Mrisho.

Kuhusu mchezo dhidi ya Uhamiaji FC, Mrisho alisema ulikuwa mgumu katika dakika zote licha ya kupata ushindi huo mnono.

Aliongeza wachezaji wake walijituma wakati wote ili kuhakikisha wanamaliza mechi mapema.

"Wachezaji wanaasilimia kubwa katika ushindi tunaopata, kubwa kujituma kwao, lakini pia mashabiki wetu wanahamasa kubwa sana, hatutegemei kuwaangusha katika michezo ijayo," aliongeza kocha huyo.

Aliongeza wanaendelea kujiimarisha kuelekea mechi yao inayofuata dhidi ya Mlandege itakayochezwa Oktoba 21, mwaka huu.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayofanyika kila mwaka kwa kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

**Wachezaji wanaasilimia kubwa katika ushindi tunaopata, kubwa kujituma kwao, lakini pia mashabiki wetu wanahamasa kubwa sana, hatutegemei kuwaangusha katika michezo ijayo.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### AMORIM KUMRITHI GUARDIOLA

KLABU ya Manchester City inamfikiria Kocha Mkuu wa Sporting, Ruben Amorim, mwenye umri wa miaka 39, kuwa kocha wao mpya ikiwa Pep Guardiola (53), ataondoka mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu.***(Guardian)***

#### DAVIES ATAJWA UNITED

MLINZI wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Canada, Alphonso Davies, mwenye umri wa miaka 23, analengwa na Manchester United msimu ujao. ***(Sky Germany)***

#### CHUKWUEMEKA ANUKIA BARCA

BARCELONA inaweza kuwalenga kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romeo Lavia na kiungo mshambuliaji wa England, Carney Chukwuemeka, wote wana umri wa miaka 20, kutoka Chelsea Januari. ***(Sport)***

#### K AIVURUGA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak, mwenye umri wa miaka 25 ameiweka Arsenal katika hali ya tahadhari huku akiendelea kusuasua kusaini mkataba mpya na mabosi wake wa Newcastle. ***(talkSPORT)***

#### KOUYATE AKARIBIA LEEDS

KIUNGO wa kati wa Senegal, Cheikhou Kouyate, mwenye umri wa miaka 34, alifanyiwa vipimo vya afya huko Leeds Jumanne iliyopita kama mchezaji huru baada ya kuondoka Nottingham Forest. ***(Football Insider)***

#### PSG YAMHITAJI RASHFORD

KLABU ya Paris Saint-Germain bado imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 26, kutoka Manchester United.***(TeamTalks)***

#### CHELSEA: NKUNKU HAONDOKI

CHELSEA haiko tayari kukaribisha ofa kwa mshambuliaji wa Ufaransa, Christopher Nkunku, mwenye umri wa miaka 26, huku akihusishwa na Paris St-Germain. ***(Football Insider)***

#### HARALDSSON AGEUKA LULU

KLABU za Tottenham Hotspur na Crystal Palace zote zinamtaka winga wa Lille ya Ufaransa, Hakon Arnar Haraldsson, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Football Transfers)***

#### GARCIA NJIA MOJA

KIPENGELE cha kutolewa kwa mlinda mlango wa Espanyol, Mhispania Joan Garcia, 23, ambaye alikuwa anatakiwa na Arsenal majira ya joto, kimepunguzwa hadi euro milioni 25. ***(Mundo Deportivo)***

#### HAALAND KUVUNJA REKODI

KLABU ya Manchester City huenda ikadai ada ya uhamisho wa rekodi ya dunia kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland, 24, ili kujiunga na Real Madrid au Barcelona. ***(Teamtalks)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




**BUENOS AIRES,** Argentina

### Nahodha huyo wa Argentina asema anafurahia sana akicheza...

LIONEL Messi alionyesha mchezo mwingine wa hali ya juu kwa Argentina, akifunga hat-trick na kuongeza pasi mbili za mabao katika ushindi mnono dhidi ya Bolivia kwenye mechi ya kufuzu Kombe la Dunia kwa ukanda wa Amerika Kusini iliyochezwa jana lfajiri na akasema muda wake wa kucheza unakaribia mwisho.

Baada ya Argentina kupata ushindi wa mabao 6-0 mbele ya umati wa watu waliojazana kwenye Uwanja wa Monumental de Nuñez, mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2022 alisema anajaribu kufurahia kila wakati akiwa na timu ya taifa na kukiri mwisho wa siku zake za kucheza upo karibu.

> **"Inapendeza sana kucheza hapa nikihisi mapenzi ya mashabiki wa Argentina," alisema Messi baada ya mchezo huo.**

"Inanitia hisia kuwasikiliza jinsi wanavyopiga kelele jina langu. Sote tunafurahia uhusiano huu na mashabiki na tunapenda kucheza nyumbani."

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake na kama angeisaidia Argentina kutetea taji lao kwenye Kombe la Dunia litakalofanyika mwaka 2026, Messi alikuwa mwangalifu na mkweli kwa jibu lake.

"Sikuweka tarehe ya mwisho kuhusu mustakabali wangu," alisema Messi.

"Ninafurahia haya yote. Nina hisia zaidi kuliko hapo awali na kuchukua upendo wote kutoka kwa watu kwa sababu najua hii inaweza kuwa mchezo yangu ya mwisho."

Nyota huyo, ambaye alikosa raundi mbili za michuano hiyo iliyochezwa Septemba kwa sababu ya jeraha la kifundo cha mguu wa kulia, alicheza kuanzia mwanzo hadi mwisho na kuongeza kwenye kitabu chake cha historia katika mchakato huo. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Messi kuandikisha mabao mengi na kusaidia katika mchezo mmoja katika timu ya taifa, na hat- trick hiyo, iliyomfanya afikishe mabao 112.

Bao la kwanza la Messi lilipatikana baada ya makosa ya beki wa Bolivia, ambaye alikosa pasi na kumruhusu Messi mwenye umri wa miaka 37 kukimbia kwa uhuru na kumaliza bila shida mbele ya kipa, Billy Viscarra.

Messi alisaidia bao la Lautaro Martínez dakika ya 42 na kutoa pasi ya uhakika kwa mara nyingine tena katika muda wa nyongeza kwenye goli lililofungwa na Julián Álvarez.

Argentina walionekana kupunguza kasi yake baada ya mapumziko lakini wakafunga tena kupitia Thiago Almada dakika ya 69.

Onyesho la Messi lilikuwa na miguso miwili mikubwa ya umaliziaji kutoka pembeni mwa eneo la hatari, ya kwanza dakika ya 84 na ya pili dakika ya 86, na furaha ilionekana kwenye uso wake.

"Ni furaha kuwapo na kuthamini wakati huu. Kuzungukwa na wachezaji wenzangu wadogo, kutokana na umri wangu, kunanifanya nijisikie kama mtoto tena," alisema Messi.

Matokeo hayo yamewafanya mabingwa hao wa Kombe la Dunia kuwa vinara wakiwa na pointi 22 baada ya mechi 10, pointi tatu mbele ya Colombia walio nafasi ya pili, ambao awali waliilaza Chile 4-0. Uruguay iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 16 baada ya kutoka sare tasa na Ecuador.

# MBAPPÉ AKANA MADAI YA UBAKAJI




**PARIS,** Ufaransa

MADAI ya ubakaji dhidi ya nahodha wa Ufaransa na fowadi wa Real Madrid, Kylian Mbappé, ni "uongo kabisa" na "uvumi wa kashfa," wawakilishi wake wamesema ripoti za vyombo vya habari alikuwa anachunguzwa kuhusu tukio katika hoteli ya Stockholm siku ya Jumanne.

Waendesha mashtaka wa Sweden walithibitisha katika taarifa yao wakijibu taarifa za vyombo vya habari uchunguzi wa madai ya ubakaji katika hoteli moja mjini Stockholm ulifunguliwa, lakini hawakumtambua mshukiwa.

Mtangazaji wa televisheni ya SVT na Dailies Expressen na Aftonbladet, alinukuu vyanzo ambavyo havikutajwa, viliripoti Mbappé, mwenye umri wa miaka 25, alikuwa mshukiwa katika kesi hiyo.

"Uvumi mpya wa kashfa unaanza kuwasha mtandao," taarifa iliyotumwa kwa Reuters na wawakilishi wa Mbappé katika kampuni ya mahusiano ya umma, Patricia Goldman, ilisema.

"Tuhuma hizi ni za uongo kabisa na hazijibiki, na uenezaji wao haukubaliki.

"Kylian Mbappé hatavumilia kwa hali yoyote uadilifu, sifa na heshima yake kuchafuliwa na minong'ono isiyo na msingi."

"Hatujui malalamiko ni dhidi ya nani, sijui kama malalamiko yanamlenga yeye," wakili wa Mbappé, Marie-Alix Canu-Bernard, alikiambia kituo cha televisheni cha Ufaransa TF1 Jumanne.

"Kamwe hayuko peke yake, hajawahi kukabiliwa na hali ya hatari. Haijumuishi kabisa inaweza kuwa na tabia yoyote ya kulaumiwa kwa upande wake. Ni uhakika kabisa. Yeye ni mtulivu lakini anashangazwa na hasira ya vyombo vya habari.

"Hajafanya chochote kibaya," Canu-Bernard alisema, akiongeza Mbappé atashirikiana na mfumo wa haki wa Sweden ikiwa atalengwa moja kwa moja na uchunguzi.

# Tuchel rasmi kocha mpya England



**LONDON,** England

CHAMA cha Soka England (FA), kimemtangaza rasmi, Thomas Tuchel, kuwa kocha mpya wa Timu ya Taifa ya wanaume.

FA imetangaza pia Tuchel atasaidiwa na Anthony Barry.

Tuchel anakuwa kocha wa tatu mzaliwa wa kigeni na Mjerumani wa kwanza kuchukua mikoba ya kuinoa England huku msaidizi wake, Barry akiwa ni raia wa nchi hiyo.

Lee Carsley, ambaye alikuwa Kaimu Kocha Mkuu tangu, Gareth Southgate, alipoondoka Julai, mwaka huu, ataendelea kuiongoza England katika michezo yake miwili itakayofanyika Novemba, halafu atarejea katika kikosi cha U-21.

Southgate alijiuzulu baada ya miaka nane ya kushindwa kwa England katika michuano ya Euro 2024 dhidi ya Hispania.

Awali FA ilimteua Carsley kwa muda kwa ajili ya mechi za Ligi ya Mataifa ya Uefa huku wakiongeza kasi ya kuwatafuta wanaoweza kuwania nafasi hiyo, ambapo Tuchel alikuwa anachuana na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Carsley alikataa mara kwa mara kujitawala ndani au nje ya kuwania nafasi hiyo kwa misingi ya kudumu na huku uvumi ukiongezeka FA walikuwa na matumaini angeweza kuthibitisha anaweza kumrithi Southgate.

Vyanzo viliiambia ESPN bodi inayosimamia soka ya Uingereza ilikuwa inawasiliana na njia mbadala za hali ya juu.

Tuchel amekuwa hana kazi tangu alipoondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu uliopita, lakini alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea mwaka 2021.

Januari wakati wa mahojiano ya kipekee na ESPN, Tuchel aliulizwa ikiwa alihisi kuthaminiwa zaidi nchini England badala ya kwao Ujerumani.

"Ndiyo," alijibu. "Ninahisi tunakosoa sana wenzetu Ujerumani na haswa na wachezaji au makocha na sio tu na mimi." Swali rahisi sana. ... Nilihisi kuthaminiwa zaidi huko England."

# Adebayor afunguka Nigeria

**LAGOS,** Nigeria

MAGWIJI wa soka Afrika, Emmanuel Adebayor na Pierre Emerick-Aubameyang wameguswa na hali ya wachezaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, waliotelekezwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Al Abaq nchini Libya.

Viongozi wa eneo hilo waliwaacha wachezaji wa Nigeria kwa zaidi ya saa 15 baada ya kuwasili Jumapili usiku.

Wachezaji walionekana wakilala kwenye benchi na madaktari wa timu hiyo walitoa wasiwasi juu ya afya zao kabla ya mechi.

Libya alikuwa mwenyeji wa Super Eagles katika siku ya nne ya mechi ya kufuzu kwa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025) juzi.

Walipoteza mechi ya kwanza kwa bao 1-0 huko Uyo, huku kukiwa na madai walikatishwa tamaa na mamlaka ya Nigeria kusafiri kwa barabara kutoka Port Harcourt hadi Uyo.

Super Eagles walipowasili Libya kwa mkondo wa pili, ndege yao ilitelekezwa Uwanja wa Ndege wa Al Abaq, ambapo waliachwa bila huduma kutokana na ripoti ya Daily Trust.

NFF imeachana na mechi hiyo huku Super Eagles ikirejea Nigeria, na kumwacha Adebayor akijiuliza maswali.

"Tabia ya aina hii haikubaliki kwa maendeleo ya soka la Afrika. Hakuna timu inayopaswa kukabiliana na hali kama hiyo. Tunasimama na Super Eagles ya Nigeria. Heshima na mchezo wa haki lazima iwe ya kwanza ndani na nje ya uwanja," aliandika Adebayor katika kurasa zake za mitandao ya kijamii.

Gwiji wa Gabon na nyota wa zamani wa Arsenal, Aubameyang aliandika katika ukurasa wake wa X, hali ile haipaswi kutokea mwaka 2024.



HABARI MICHEZO

# SINGIDA YANOGEWA KILELENI BARA, YAITAMBIA NAMUNGO

Na Adam Fungamwango

SINGIDA Black Stars imesema imeshaonja 'utamu' wa kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara hivyo haitakuwa rahisi kushushwa kwa sababu wanataka kuendelea kung'ang'ania kwenye nafasi hiyo kwa kupata ushindi watakapocheza dhidi ya Namungo Jumapili kwenye Uwanja wa Liti mkoani, Singida.

Singida Black Stars iko kileleni ikiwa na pointi 16 lakini imecheza michezo mingi zaidi ikifuatiwa na Simba yenye pointi 13 sawa na Fountain Gate FC huku mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 12 wakiwa nafasi ya nne.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, amesema jana, wamepata bahati kubwa ya kukaa kwa muda mrefu kileleni huku ligi ikisimama kutokana na Kalenda ya Kimataifa, wanataka kubakia kwenye nafasi hiyo na wataonyesha vitendo kwa kuwafunga Namungo.

"Tunashauku ya kuhakikisha tunaendelea kuongoza ligi kwa muda mrefu na hata hadi mwisho wa msimu, tumekuwa huko tangu mapumziko ya kalenda ya FIFA, hiyo ni hamasa tosha kwa wachezaji, tumeshawaambia kukaa namba moja si kazi, kuhakikisha tunaendelea kukaa pale ndiyo kazi kubwa," alisema Massanza.

**Alitamba wamejipanga vyema kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo ili kutengeneza wigo kwa timu nyingine ambazo zinawakimbiza.**

"Tunajiandaa kwenda kutafuta pointi tatu dhidi ya wageni wetu Namungo, tutacheza kwenye uwanja wa nyumbani hivi sasa maandalizi yanaendelea," Massanza alisema.

Singida Black Stars ambayo imeshinda mitano na sare moja, ikifunga magoli tisa na kuruhusu nyavu zake kuguswa mara tatu.

Timu hiyo pia inaongoza kwa kuzoa pointi nyingi zaidi kuliko timu yoyote ya Ligi Kuu ikicheza viwanja vya ugenini, ikijizolea pointi 12, ambapo imecheza michezo minne nje ya nyumbani kwake, Liti Singida, ikishinda yote, huku michezo miwili ya nyumbani ikishinda mmoja na sare moja.

## Simba, Yanga hatari zaidi maeneo haya

INATOKA UKURASA 24

wa Simba kuongeza umakini pale faulo za Yanga zinapopigwa kuelekea langoni kwao, wapinzani wao wakiongozwa na Bacca, wanaonekana wana uwezo mkubwa wa kuunganisha mipira hiyo iliyokufa.

Wakati huo huo, Kampuni ya Ujenzi ya Knauf imeingia mkataba wa mwaka mmoja na Simba ambayo hivi karibuni itashiriki hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mkurugenzi wa Knauf wa Kanda Afrika Mashariki, Ilse Boshoff, alisema jijini jana uhusiano huo na Simba ni mkubwa na utakuwa na faida kwa pande zote mbili kitaifa na kimataifa.

"Tupo nchi zaidi ya 90 duniani na malengo yetu ni kuzidi kujitanua zaidi, matumaini yetu uhusiano huu na Simba utakuwa msaada kwetu kuendelea kujulikana huku tukiendelea kuzalisha bidhaa bora za ujenzi kutoka Ujerumani," alisema Boshoff.

Naye Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, alisema mkataba huo utakuza chapa ya Knauf pamoja na Simba na kuongeza hawakuangalia thamani yake bali umuhimu wa kuendelea kujitangaza kimataifa.

"Sisi kama Simba hatukuangalia zaidi thamani ya mkataba bali tumeangalia kujitangaza na kuyavutia makampuni mengine ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza kwetu na tunawakaribisha," alisema Mangungu.

## MINZIRO ATUA RASMI PAMBA JIJI

Na Adam Fungamwango

KOCHA mkongwe nchini, Fred Minziro, ametangaza kubeba mikoba ya kuiongoza Pamba Jiji FC ya Mwanza ambayo imetangaza rasmi kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Goran Copunovic.

Mserbia huyo amehudumu katika kikosi cha Pamba Jiji kwa miezi miwili.

Mwenyekiti wa Pamba Jiji, Biko Khotecha, amesema Minziro, ambaye ni mmoja wa makocha wenye uzoefu na soka la Tanzania atasaidiwa na kocha wa vijana chini ya miaka 20 wa timu hiyo, Mathias Wandiba.

"Bodi ya Wakurugenzi ilikaa na uamuzi uliotolewa ni Kocha Mkuu wa Pamba Jiji sasa atakuwa ni bwana Minziro, nimeambiwa atakuwa ndiye mkuu wa benchi la ufundi, hii ndiyo habari rasmi.

Kwa maana hiyo mashabiki wetu waelewe klabu yao imeachana na Goran, kitu chochote kitakachotokea baada ya hapa tutafahamishana, lakini hii ndiyo habari sahihi na kesho (leo), Minziro ataanza kazi kwenye Uwanja wa Nyamagana," alisema mwenyekiti huyo.



Goran, kocha wa zamani wa Simba na Tabora United, aliiongoza Pamba kwenye michezo saba ya Ligi Kuu bila kupata ushindi, ikitoa sare nne, kupoteza mitatu, ikiburuza mkia na pointi zake nne.



Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu (kulia), na Mkurugenzi wa Kanda Afrika Mashariki ya Knauf, Ilse Boshoff, wakiwa wameshika nakala za mikataba baada ya kampuni hiyo kuingia makubaliano ya kuidhamini klabu hiyo kuelekea hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: SIMBA SC**

## Stars: Nafasi kufuzu AFCON bado tunayo

INATOKA UKURASA 24

pamoja na wachezaji wake kujitahidi 'kutoa jasho lao lote' uwanjani, lakini walihukumiwa na ukosefu wa umakini dakika za mwishoni.

Hata hivyo aliwapongeza DR Congo kwa jinsi walivyocheza na hiyo imetokana na kikosi chao kuundwa na wachezaji wazuri kwenye uwezo wa kuamua mechi, ingawa hilo halikuwafanya nyota wake kuvunjika moyo, watapambana mpaka dakika za mwisho.

Naye mshambuliaji wa DR Congo, Fiston Mayele, alisema sababu iliyowafanya wapate ushindi ni kuizidi mbinu na ubora Taifa Stars.

Mayele alitaja sababu nyingine iliyowapata pointi sita dhidi ya Taifa Stars ni kukosekana katika kikosi hicho, winga wa kimataifa, Simon Msuva.

"Tulikuwa tuna hofu sana na Msuva pamoja na Samatta (Mbwana), hata kocha wetu alikuwa anafuatilia nani na nani wataitwa kwenye Timu ya Tanzania, Msuva ana kasi na anajua kukimbia kwenye 'space' (nafasi), kama angekuwa na Samatta pale mbele tungekuwa kwenye hatari zaidi, sijui ni kwanini hajaitwa," alisema Mayele.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga alisema Samatta alikuwa ni mchezaji wanayemhofia zaidi kwenye mechi zote mbili walizocheza.

"Amecheza vizuri sana katika mechi zote, anajua kukaa na mpira na ni mgumu kumpokonya, nadhani kama angekuwa na Msuva kazi kwetu ingekuwa ngumu kidogo, lakini tumefurahi kupata ushindi na kufuzu AFCON," alisema nyota huyo anayecheza Pyramid ya Misri.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 17, 2024

Nipashe



**'Muda wangu unaelekea ukingoni'** UKURASA 21



Nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta (kulia), akimtoka beki wa DR Congo, Henock Inonga (aliyelala), katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Stars ililala mabao 2-0. **PICHA: TFF**

## Stars: Nafasi kufuzu AFCON bado tunayo

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Suleiman 'Morocco' akisema Tanzania bado ina nafasi ya kufuzu kucheza fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), wapinzani wao Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), waanika walikuwa wanamhofia zaidi nyota, Simon Msuva.

Taifa Stars ilikubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa DR Congo ambayo ni kinara wa Kundi H ilifikisha pointi 12 inafuatiwa na Guinea yenye pointi sita baada ya kuichapa Ethiopia mabao 3-0 na Stars iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne kibindoni.

Mabao yote mawili ya DR Congo yalifungwa na nyota anayechezea Young Boys ya Uswizi, Meshack Elia, ambaye aliingia akitokea benchi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kumalizika, Morocco alisema hawajakata tamaa ya kufuzu AFCON na anawasihi Watanzania kutovunjika moyo kwa sababu kufungwa mchezo huo wa juzi si mwisho wa safari yao.

Morocco alisema sababu kubwa iliyopelekea kupoteza mchezo huo wa jana ilitokana na viwango vya mchezaji mmoja mmoja kwa timu hizo mbili.

Kocha huyo alisema

INAENDELEA UKURASA 23

### KUELEKEA DABI

# SIMBA, YANGA HATARI ZAIDI MAENEO HAYA

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Maxi aonekana mwiba, Wajerumani waipa Msimbazi...

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya mechi ya watani wa jadi, vigogo hao wa soka nchini wameonekana kuwa na sifa tofauti za kuleta hatari na kufunga mabao msimu huu, Wekundu wa Msimbazi wanaonekana hatari zaidi wanapoingia ndani ya eneo la hatari, huku Yanga wao hawana masihara kwa kupiga mashuti kutoka mbali.

**Mbali na hilo, mabao ya Simba msimu huu inaonekana kupata mabao mengi wakitumia mipira ya pembeni, krosi, huku Yanga ikifunga kwa pasi za kupenyeza pamoja na faulo.**

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, Simba ambao mpaka sasa imepachika mabao 12 katika Ligi Kuu Tanzania Bara, magoli yake 11 wameyafunga na wachezaji wakiwa ndani ya boksi.

Wachezaji wa Simba waliopachika mabao hayo ndani ya boksi ni pamoja na Che Fondoh Malone, Valentino Mashaka, Awesu Awesu, Edwin Balua, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoua (amefunga mawili), Leonel Ateba (amepachika pia mawili), Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na Fabrice Ngoma.

Kwa maana hiyo, mabeki wa Yanga wanatakiwa kutowaruhusu wachezaji wa Simba kuwa huru na mpira wanapokuwa ndani ya eneo la hatari. Mabao sita, ambayo ni nusu ya mabao yote ya timu hiyo yamefungwa na faulo tatu zilizopigwa na Ahoua mara mbili, Zimbwe Jr na Shomari Kapombe.

Iwapo mabeki wa Yanga wanataka kuwadhibiti Simba ili wasifunge, wanapaswa pia kuchunga maeneo yao ya pembeni kutowaruhusu kutembea sana huko, kwa sababu wanaonekana ni hatari na mpango mkakati wao wa mabao unatokea huko.

Kwa upande wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wanaonekana ni hatari zaidi kufunga mabao wakiwa nje ya eneo la hatari.

Wakati Simba wana bao moja tu wakifunga nje ya boksi, likiwekwa na Mashaka, Yanga wana mabao mawili waliyofunga wakiwa nje ya hatari, tena yote yakifungwa na Mkongomani Maxi Nzengeli.

Kiungo huyo mwenye mabao matatu, mawili akipachika akiwa nje ya eneo la hatari, akifanya hivyo, Agosti 29, mwaka huu, Yanga ilipoifunga Kagera Sugar mabao 2-0, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera na Oktoba 3, mwaka huu walipoichakaza Pamba Jiji magoli 4-0.

Kwa takwimu hii, inaonyesha licha ya Yanga kuwa na mabao mengi ya nje ya boksi kuliko wapinzani wao Simba, lakini Maxi ndiye mchezaji wa kuchungwa na mabeki wa Wekundu wa Msimbazi, asitazame mapana ya lango akiwa mbali. Ndiye mchezaji aliyefunga bao katika mchezo wa mwisho timu hizo zilipokutana Agosti 8, mwaka huu kwenye mechi ya Ngao ya Jamii, Simba ikilala kwa bao 1-0.

Wakati pia Simba ikiwa haina bao lolote kwa faulo ya moja kwa moja, au lililopatikana kwa kuunganishwa kwa mpira hiyo, Yanga ina mabao mawili yaliyotokana na mipira ya adhabu.

Ingawa si ya faulo ya moja kwa moja, lakini mipira iliyopigwa na Stephane Aziz Ki na Nzengeli, yote ilitua kichwani kwa beki, Ibrahim Hamad 'Bacca' na kuiweka wavuni katika michezo miwili tofauti.

Ilikuwa ni katika mchezo wa kwanza uliochezwa ni Septemba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya Yanga ikishinda bao 1-0 dhidi ya wenyeji KenGold, na Oktoba 3, mwaka kwenye Uwanja wa Azam Complex, Yanga ikiichapa bila huruma Pamba Jiji mabao.

Hili ni angalizo kwa wachezaji

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >